




## Daktari auawa kwa kukatwa mapanga na kuporwa pikipiki

UKURASA 3




UKURASA 9

Jumapili Mei 7, 2023 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

JUMAPILI

www.ippmedia.com

ISSN 0856 • No. 0581303

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US

# Polisi, Mkemia, DPP kuchunguza kifo cha mwanafunzi UDOM



UKURASA 2



SACP David Misime

DPP Sylivester Mwakitalu

UKURASA 4

## Waziri awaonya wanawake jeuri, kujikweza kisa vyeo na kipato





## Kimiti asimulia anguko wanasiasa waliomzodoa aking'atuka ubunge

UK. 2

MICHEZO SIMBA, AZAM MECHI YA KISASI UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

HABARI KITAIFA

# Polisi, Mkemia, DPP kuchunguza utata kifo mwanafunzi UDOM

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi nchini kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), wameingilia sakata la utata wa kifo cha mwanafunzi Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), Nusura Abdallah, na kutangaza kuanza uchunguzi.

Baada ya kifo cha binti huyo, kuliibuka mjadala wenye utata huku kikihusishwa na ajali aliyoipata Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk. Festo Dugange.

Kwa mujibu wa taarifa ya jeshi hilo iliyotolewa jana na Msemaji wake, Kamishna Msaizidi Mwandamizi (SACP) David Misime, wameona mjadala katika mitandao ya kijamii kuhusu kifo cha mwanafunzi huyo, kilichotokea mkoani Kilimanjaro.

"Taarifa hizo zimekuwa zikihusisha kifo hicho na ajali iliyotokea jijini Dodoma Aprili 26, mwaka huu, iliyomhusisha Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Dk. Festo Dugange, lakini pia zikidaiwa kimetokana na kipigo kutoka kwa mpenzi wake.

"Jeshi la Polisi lingependa kutoa ufafanuzi kuwa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro baada ya kuona taarifa hizo kupitia mitandao ya kijamii na sababu zilizotolewa, wameshaanza uchunguzi kwa watu mbalimbali," alisema.

Misime alisema uchunguzi huo pia unahusisha hospitali alikotibiwa binti huyo na washirikiana na Ofisi Mkemia Mkuu wa Serikali, DPP na wadau wengine wa haki jinai.

Alisema Jeshi la Polisi linatoa wito kwa mtu yeyote mwenye taarifa sahihi na zenye ukweli, asisite kulipatia jeshi hilo ili kuharakisha uchunguzi.

"Jeshi la Polisi linasisitiza kuwa uchunguzi wa tukio hili ukikamilika taarifa kamili ya kilichobainika kitatolewa kwa umma kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu za nchi," alisema.

Taarifa iliyotolea juzi kwa umma na Kitengo cha Masoko na Mawasiliano cha UDOM, ilisema kwenye mitandao ya kijamii kumekuwa na taarifa zisizo rasmi kuhusu mwanafunzi huyo na kutoa taarifa yao waliyoiita kuwa ndiyo rasmi.

"Nusura alikuwa mwanafunzi Shahada ya Kwanza ya Sanaa katika Elimu (BA-Ed) katika Ndaki ya Insia na Sayansi za Jamii UDOM.

"Taarifa zinaonyesha kwamba hadi kufikia jioni Aprili 27, mwaka huu, alionekana chuoni akiendelea na masomo kama kawaida.

Mei 3, mwaka huu, Menejimenti ya Chuo ilipokea taarifa kwa mwanafunzi ambaye alikuwa anasoma naye kuwa amepokea taarifa kutoka kwa mtu anayejitambulisha kuwa ni mjomba wake Nusura," ilisema taarifa hiyo.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, mjomba huyo alikuwa akimjulisha mwanafunzi huyo kwamba Nusura amefariki dunia akiwa anapatiwa matibabu katika Hospitali ya Faraja iliyoko Himo, Kilimanjaro.

"Tukizingatia kwamba masomo yanaendelea, Menejimenti ya Chuo ilifanya juhudi za kutafuta taarifa za ziada na kufanikiwa kumpata dada yake Nusura anayeishi Uchira, mkoani Kilimajaro ambaye alidhibitisha kutokea kwa kifo cha mdogo wake.

"Taarifa zaidi zilieleza kuwa mwili wa marehemu ulisafirishwa Mei 3, mwaka huu, kutoka Moshi hadi nyumbani kwao Iramba, mkoani Singida," ilisema.

Taarifa hiyo ilisema baada ya chuo kujiridhisha, utaratibu ulifanyika kwa kushiriki na kutoa salamu za pole kwa familia anapo maziko yake yalifanyika Mei 4, mwaka huu.



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango akisalimiana na Rais wa Burundi, Evariste Nayishimiye baada ya kuwasili katika Ikulu ya Bujumbura, nchini humo jana. Makamu wa Rais, amemwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan katika Mkutano wa 11 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Nchi Wanachama wa Mpango wa Amani, Usalama na Ushirikiano kwa ajili ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo na Ukanda wa Maziwa Makuu. **PICHA: OMR**

# Kimiti asimulia anguko la waliomzodoa aking'atuka

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MWANASIASA mkongwe nchini, Paul Kimiti, amesimulia anguko la wanasiasa waliomzodoa alipotangaza kung'atuka ubunge mwaka 2010.

Amesema wale waliong'ang'ania, walijikuta wakianguka kwenye uchaguzi mkuu uliofuata mwaka huo.

Akizungumza jana jijini hapa kwenye Kongamano la Kumbukizi ya miaka 101 ya kuzaliwa kwa Mwalimu Julius Nyerere, lililoandaliwa na Taasisi ya Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Kimiti alisema mwaka 2010 alifuata falsafa ya Mwalimu Nyerere ya kung'atuka bila kusubiri kushambuliwa kwa maneno na watu.

Kimiti ambaye ni Mwenyekiti wa taasisi hiyo, alisema: "Wenzangu walinilaumu sana ndani ya Bunge wakasema Mzee Kimiti unatushtaki kwa sababu unavyosema hivyo watasema Mzee Kimiti ametoka wewe unangoja nini? Nikasema shauri yenu. Lakini wengi waliporomoka kwenye uchaguzi wale waliong'ang'ania."

Kimiti alisema kinachomfanya aishi kwa amani ni kitendo chake cha kutoka kwa amani na utulivyo na sasa ana umri wa miaka 83.

"Namshukuru Mungu ananilinda, wenzangu wamechoka sana nilisema Mungu ana sababu yake," alisema kuhu akiomba serikali kujenga makumbusho ya Mwalimu Nyerere Dodoma ili kuwe mahali pa utalii.

"Dodoma iwe mahali pa utalii. waangalie historia ya Baba wa Taifa. Tunataka tupate eneo la zaidi ya ekari 300 ili taasisi mbalimbali ziweke vitu vyake, kuwe na mifugo, wanyama, michezo.

Tumeona wazee tuliseme mapema hatutatumia fedha za serikali, wapo wafadhili watatoa," alisema.

Kimiti alisema falsafa anayotumia na kuishi nayo ni kutumia vidole vitano yaani 'kuwa Karibu na wenzako, kaa vizuri na watawala, usidharau watoto wasaidie'.

"Watawala, wabunge tukifanya kazi kama timu moja tutafanya maajabu,"alisema.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alipongeza taasisi hiyo inayolenga kuwafikia vijana ili kuwa na uelewa mpana kazi zilizofanywa na waasisi.

Alisema kuna mambo ambayo vijana wanapaswa kufahamu ni kumfahamu na kumwelezea Mwalimu Nyerere, kipaji chake katika harakati za kupigania uhuru, kutambua juhudi katika harakati za kuleta amani, kuimarisha ustawi wa Tanzania na maisha ya Nyerere.

Majaliwa alitoa wito kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kuandaa utaratibu utakaosaidia vijana kujifunza na kumfahamu Mwalimu Nyerere.

"Katika uhai wa Mwalimu katika uongozi wake alisisitiza masuala haya kama urithi na falsafa zake, alisisitiza kupinga ukabila alikemea kila wakati, udini ni jambo alisisitiza na kuasa viongozi wasitafute uongozi kwa kigezo cha udini.

"Tusiingie huko kwenye masuala ya ukabila na udini, jambo jingine kupambana na ujinga, maradhi na umasikini, maadili ya uongozi na kupinga rushwa, alisisitiza Mwalimu viongozi safi wasiopenda rushwa na rushwa ndio adui wa maendeleo yetu,"alisema.

Alisema katika harakati za kisiasa za Mwalimu alitamani kuunganisha nchi na kuwa na uongozi wa pamoja na ndio mafanikio ya Tanganyika na Zanzibar.

"Tunashuhudia falsafa zake zinaishi na ni jukumu letu sisi kuyaendeleze ili vizazi vijavyo viishi na falsafa hizi, taasisi hii haifungamani na itikadi yeyote ya siasa lengo ni kuendeleza umoja, ustawi wa watanzania,"alisema.

Alitoa wito kwa mamlaka mbalimbali kushirikiana na taasisi hiyo katika kutoa elimu ya falsafa ya Mwalimu Nyerere, uzalendo na juhudi hizo zitachangia kupambana na maovu ikiwamo rushwa.

Kadhalika, alisema Mwalimu Nyerere alizungumzia suala la mmonyoko wa maadili, malezi ya watoto, mila na tamaduni za watanzania.

"Sote tuna wajibu wa kuhakikisha tunakuwa na kizazi salama kinachozingatia mila, desturi na tamaduni zinazoheshimu utu na kuimarisha mshikamano wa kitaifa, tuendelee kuenzi mila desturi na tamaduni na kuzingatia sheria za nchi," alisema huku akibainisha kwamba serikali itaendelea kuchukua kwa wote watakaobainika kufanya vitendo kinyume na maadili ya taifa.

"Niwaombe wazazi, walezi na jamii kuimarisha mahusiano na urafiki na watoto ili kupata viashiria vya vitendo vya ukatili dhidi ya watoto, viongozi wa dini tunaendelea kuwaomba kuwakumbusha waumini kuzingatia maadili na malezi ya watoto,"alisema.

HABARI KITAIFA

# Daktari auwawa kisha kuporwa pikipiki

**Na Samson Chacha,** TARIME

DAKTARI Isack Daniel wa Kituo cha Afya Kerende katika Halmashauri ya Wilaya ya Tarime, ameuawa kwa kukatwa mapanga sehemu mbalimbali za mwili kisha wauaji kupora pikipiki yake.

Kamanda wa Mkoa wa Kipolisi Tarime/Rorya, Kamishna Msaidizi (ACP) Geofrey Sarakikya, alisema juzi kuwa tukio hilo lilitokea usiku wa kuamkia Mei 4, mwaka huu.

ACP Sarakikya alisema baada ya watu hao kutekeleza mauaji hayo, waliutelekeza mwili wa daktari pembezoni mwa barabara.

Alisema mwili huo ulitambuliwa na wananchi baada ya kumkuta tayari amefariki dunia akiwa na majeraha katika maeneo mbalimbali ya mwili pamoja na kitu chenye ncha kali pembeni mwake.

Pia alisema wananchi hao pamoja na wanafamilia wa marehemu, walilieleza Jeshi la Polisi kuwa wakati wa tukio hilo, Dk. Daniel alikuwa na pikipiki ambayo iliporwa na watu hao.

"Tunaendelea na uchunguzi zaidi kuhusiana na kifo cha daktari huyo na tunaendesha msako ili kubaini kila mmoja aliyehusika na uhalifu huu. Tunawaomba pia wananchi kutoa ushirikiano kwa kuwafichua wahalifu hao ili sheria ichukue mkondo wake," alisema.

Diwani wa Kemambo, Rashid Bogomba, alisema kutokea kwa tukio hilo la mauaji kumesababisha pengo kwa wakazi wa eneo hilo kutokana na daktari huyo kuwa na mchango mkubwa katika kutoa huduma za afya kwa wananchi wa eneo hilo.

Diwani huyo alilaani tukio hilo na kuliomba Jeshi la Polisi kufanya uchunguzi na kuwabaini mapema wahusika ili kuondoa hofu ambayo imetanda kwa wakazi wa kata hiyo.



Naibu Waziri wa Madini, Steven Kiruswa (kulia), akimsikiliza Mwekezaji wa kampuni ya Digalla inayochimba madini ya Gypsum, Joseph Mushi (wa pili kulia), baada ya kumaliza mgogoro uliojitokeza kati ya kampuni hiyo na ya Kitivo Investment, katika tarafa ya Makanya, wilayani Same, mkoani Kilimanjaro mwishoni mwa wiki. **PICHA: ASHRACK MIRAJI**

# CAG abaini ukosefu kanzidata ya taifa kuhusu viumbe vamizi

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), amebaini kuwapo kwa udhibiti usiotosheleza wa viumbe vamizi katika mazingira nchini, huku taasisi zilizopewa dhamana zikishindwa kuandaa kanzidata ya taifa ya viumbe vamizi.

Katika ripoti yake ya 2021/22 iliyowasilishwa Bungeni mwezi uliopita, CAG Charles Kichere, amebaini Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira, kwa kushirikiana na Wizara za kisekta, haikuchukua hatua zenye tija za kudhibiti viumbe vamizi nchini.

CAG anasema katika Ripoti ya Mwaka ya Ukaguzi wa Ufanisi ya Mwaka 2021/22, hali hiyo inadhihirishwa na ukweli kwamba, taasisi hizi hazikuandaa kanzidata ya taifa ya viumbe vamizi.

Aidha, CAG anasema kutokana na kukosekana kwa kanzidata hiyo, nchi inakosa taarifa za kina kuhusu viumbe vamizi, ambavyo vimeingia na kuenea katika maeneo mbalimbali, hivyo nchi ina hatari kubwa ya kukosa namna bora ya kufuatilia kukua na kuenea kwa aina mbalimbali za viumbe vamizi.

Kuhusu usimamizi wa viumbe vamizi katika mazingira ya nchikavu, CAG anasema ukaguzi ulibaini uwepo wa jitihada zilizofanyika, ambapo serikali iliweka mipango mbalimbali inayolenga kuhakikisha kuna udhibiti wa viumbe vamizi nchini. Katika ripoti hiyo, CAG anasema upungufu mbalimbali ulibainika ukiwamo uzuiaji usiotosheleza wa viumbe vamizi. Ukaguzi ulibaini kuwa Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira, kwa kushirikiana na wizara za kisekta, haikuchukua hatua zenye tija ili kuzuia uingiaji na ueneaji wa viumbe vamizi nchini.

Kadhalika, CAG anasema hali hii ilidhihirishwa na utambuzi na usimamizi usiojitosheleza wa njia zinazotumiwa na viumbe hawa wakati wa uingiaji na ueneaji wao.

Pia ilibainika kuwa Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira na Wizara ya Kilimo, kupitia Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu (TPHPA), hawakufanikiwa kudhibiti ipasavyo viumbe vamizi katika mipaka ya nchi

Udhibiti usiofaa huongeza hatari ya viumbe vamizi kuingia na kuenea katika mazingira husussani ya nchi kavu.

CAG anasema hali hiyo inaleta madhara katika mifumo ya ikolojia kwa kuwa inaweza kubadilisha mfumo wa haidrolojia, virutubisho, na makazi ya viumbe na hivyo kusababisha hatari ya kutoweka kwa baadhi ya viumbe hai.

Uzuiaji na udhibiti usiojitosheleza wa viumbe vamizi ulisababishwa na uratibu mdogo miongoni mwa wadau na ufuatiliaji na tathmini isiyotosheleza ya hatua za kuzuia na kudhibiti viumbe vamizi ndani ya nchi.

# WHO yatangaza UVIKO- 19 si janga la dharura kimataifa

**Na Romana Mallya**

SHIRIKA la Afya Duniani (WHO), limesema UVIKO- 19 si ugonjwa wa dharura wa afya katika jumuiya ya kimataifa.

Kutokana na taarifa hiyo, Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, kupitia ukurasa wake wa Instagram jana aliandika kuwa: "Nitumie fursa hii kuwashukuru viongozi wetu wakuu wa nchi, watumishi wa afya, asasi za kiraia. Taasisi binafsi ikiwamo WHO Tanzania na wadau wote wa maendeleo wa ndani na nje ya nchi na wananchi kwa ujumla kwa kushiriki nasi kikamilifu katika mapambano dhidi ya UVIKO-19 nchini."

Waziri Ummy alisema haikuwa kazi rahisi lakini kwa jitihada za pamoja hali imekuwa hivyo na imewezekana.

"Ninatoa pole kwa wote waliopoteza wapendwa wao kutokana na ugonjwa huu. Ninawaombea kwa Mungu wapumzike kwa amani," alisema.

Juzi, Mkurugenzi wa WHO, Tedros Ghebreyesu, alitangaza kuwa: "Kwa matumaini makubwa janga la UVIKO - 19 limekomeshwa kama dharura ya afya ya umma."

Hata hivyo, kiongozi huyo amesisitiza kwamba, hiyo haimaanishi kuwa ugonjwa huo si tishio tena duniani.

Akitoa taarifa kwa vyombo vya habari katika makao makuu ya shirika hilo, Geneva nchini Uswisi, alisema: "Wiki iliyopita, UVIKO- 19 ilikatili maisha kila baada ya dakika tatu hivyo ndivyo vile vifo tu tunavyojua."

Kwa mujibu wa na ukurasa wa virusi vya Corona wa WHO ambao umekusanya takwimu muhimu tangu mwanzoni mwa janga hilo, jumla ya wagonjwa duniani kote sasa inafikia 765,222,932 na vifo ni 6,921,614.

Hadi Aprili 30, mwaka huu, Zaidi ya dozi bilioni 13.3 za chanjo ya UVIKO -19 ziLItolewa duniani kote.

Dk. Tedros alisema bado ugonjwa huo unaua na kubadilika na kwamba uamuzi huo wa kutangaza kumalizika kwa dharura ya afya haujafanywa kirahisi.

## Serikali yataja sababu nne kuendelea vifo wajawazito

**Na Sabato Kasika**

WIZARA ya Afya imetaja sababu nne ambazo zinachangia kuendelea kuwapo kwa vifo vya wajawazito zikiwamo umaskini na umbali wa vituo vya afya.

Sababu zingine zilizotajwa na wizara ni wajawazito wenyewe kutopenda kwenda kujifungulia vituoni na wengine kuzuiwa na wenza wao.

Hayo yalisemwa juzi na Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Dk. Seif Shekilaghe, katika kongamano la maadhimisho ya Siku ya Wakunga Duniani, lililofanyika Dar es Salaam.

Akisoma hotuba kwa niaba ya Katibu Mkuu huyo, Mkuu wa Miradi wa Wizara ya Afya, Dk. Catherine Joachim, alisema bado kuna haja ya kuendelea kuelimisha wajawazito, ili itambue umuhimu wa kujifungulia katika vituo vya afya.

"Takwimu za utafiti wa demografia na afya ya mwaka 2022 zinazoonyesha kuwa pamoja uwekezeaji mkubwa uliofanywa na serikali katika afya bado la kujifungulia katika vituo vya afya ni tatizo ingawa kuna maendeleo mazuri," alisema.

Pamoja na sababu hizo, alisema idadi ya wajawazito kwenda katika vituo vya afya imeongezeka kutoka asilimia 66 ya mwaka 2015/16 hadi asilimia 85 kwa mwaka 2022 huku vifo vikitokea katika vituo hivyo vya afya.

"Pamoja na kuongezeka kwa idadi na akina mama wajawazito katika vituo vya afya pia kumekuwapo na vifo vinavyotokea vituoni vikichangiwa na sababu mbalimbali," alisema huku akitaja moja ya sababu hizo kuwa ni kutokwa damu nyingi, utoaji wa mimba na pia stadi za kuokoa maisha bado ni tatizo.

Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA) Tanzania, Mark Bryan Schreiner, alisema uwekezeaji kwenye afya ya uzazi ni wa muhimu.

"Wakunga ni watu muhimu wanatakiwa kuwekewa mazingira mazuri ya kazi kwa kulipwa vizuri, kwani taifa lenye afya, ni lazima wakunga wawe katikati, siyo chini," alisema Schreiner.

Makamu wa Rais wa Chama cha Wakunga Tanzania (TAMA), Loveluck Mwasha alisema kuna umuhimu kuongeza wakunga maeneo ya vijijini, na kwamba vituo vingi vya maeneo hayo baadhi havina wakunga na vingine vina watu wasio na utaalam.

Ukunga ni kada muhimu ambayo inahitaji kutazamwa kwa jicho la ziada ili kuhakikisha vifo vya vitokanavyo na ujawazito vinakoma.

"Tunamshukuru serikali na wadau wengine wakiwamo UNFPA, kwa jinsi tunavyoshirikina kuokoa maisha ya wajawazito," alisema Loveluck.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene (wa tatu kushoto), akikabidhi cheti cha uongozi kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Rahisi Solution Ltd, Abdirhman Ali Hassan, wakati wa mahafali ya sita ya Chuo cha Uongozi, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA.**

# Waziri aonya viongozi wanawake jeuri, kujikweza kisa vyeo, kipato

**Na Beatrice Shayo**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene, amesema wanawake kuwezeshwa kielimu na kiuchumi isiwe sababu ya kuibua jeuri na majivuno wanapopanda vyeo au kuongezeka kwa kipato.

Simbachawene aliyasema hayo juzi Dar es Salaam wakati wa mahafali ya programu za uongozi zinazotolewa na Taasisi ya Uongozi. Alisema lengo la serikali ni kuwa na viongozi watakaokuwa chachu ya maendeleo kuanzia ngazi ya familia mpaka taifa.

"Wanawake kuwezeshwa kielimu na kiuchumi isiwe sababu ya kuibua jeuri na majivuno mara mpandapo vyeo au kuongezeka kwa pato lenu. Mkifanya hivi mtaharibu juhudi za serikali," alisema.

Waziri alisema wanaamini wanawake walioelimika ni chachu ya maendeleo yenye tija kwa jamii nzima.

"Ni matumaini yangu mafunzo mliyoyapata yatawafanya kuwa chachu ya mabadiliko katika maeneo yenu ya kazi na mtakwenda kukuza na kuimarisha utawala bora wenye kufuata haki, sheria, kanuni, miongozo na taratibu tulizojiwekea. Pia yatawasaidia kuimarisha uwajibikaji, kuongeza ubunifu na kuimarisha utendaji wa kazi ili kulisaidia taifa kufikia malengo tuliyojiwekea," alisema Waziri.

Pia alisema bado kumekuwa na nafasi finyu kwa wanawake kwenye nafasi za juu za uongozi.

Alisema amefurahishwa kuwapo kwa kwa programu maalum ya mafunzo ya uongozi kwa viongozi wanawake kwa kuwa haitoshi kuwachagua, kuwateua na kuwapa nyadhifa wanawake watumishi kama hawajaelimika vya kutosha.

Waziri alisema juhudi za kukwamua wanawake lazima ziendane na kulea, kukuza vipaji vyao vya uongozi ili wanapopatiwa nafasi ili kuonyesha kwa vitendo namna gani wanawake wanaweza kubadili jamii na kuleta maendeleo.

"Nawaasa viongozi wanawake mnaohitimu mafunzo haya mkaonyeshe kwa vitendo kwa kufanya kazi kwa juhudi na maarifa, kufanya maamuzi kwa kujiamini na zaidi mkashirikane na akina baba katika utendaji," alisema Waziri.

Pia alisema suala la uratibu wa shughuli za serikali na miradi ya maendeleo umekuwa na changamoto nyingi zinazoathiri ufanisi.

"Ninatoa rai kwenu, huko muendako mkasaidie kutafuta njia bora zaidi za kuratibu utekelezakaji kwa kutumia rasimali chache na kupelekea matokeo makubwa na chanya kwa miradi ya maendeleo.

"Hatutegemei kuona mnaowaongoza au nyie wenyewe mkijihusisha na masuala ya rushwa, ubadhilifu na vitendo vya unyanyasaji ndani na nje ya kazi. Nendeni mkatende haki, mkaondoe kero kwa wananchi kwa kuboresha huduma," alisisitiza.

Awali, Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya Uongozi, Kadari Singo, alisema kuanzia mwaka 2010 hadi mwaka huu, viongozi 15,000 wamapata mafunzo ya kozi mbalimbali kwenye taasisi hiyo na matarajio yao ni kuona viongozi wengi zaidi wanajiunga katika mafunzo wanayoyatoa.

Alisema programu 200 tofauti zimetolewa kwa viongozi wa kada mbalimbali ambao wamepita kwenye taasisi hiyo na viongozi 8000 wameshiriki shughuli za taasisi kwa nyakati tofauti.

Pia alisema wameona kuna haja ya kuwa na programu maalum ya kozi kwa viongozi wanawake ambayo itawajengea uwezo viongozi hao na hatimaye kutoa fursa ya kushiriki kwenye nafasi za uongozi.

"Takwimu zinaonesha duniani ni asilimia 22 ya viongozi wanawake walioko kwenye nafasi za maamuzi na ili kufikia usawa wa asilimia 50 kwa 50 katika nafasi za uongozi itafikiwa ifikapo mwaka 2050, hivyo uwepo wa programu hii ya viongozi wanawake ni muhimu."alisema Singo.

Naye Katibu Mkuu Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Zainab Said aliipongeza Taasisi ya Uongozi kwa kuandaa programu ya viongozi wanawake kwa kuwa itasaidia kupanua wigo wa kukua na kusonga mbele katika uongozi wao ikiwemo katika nafasi za uamuzi.

Alisema taasisi hiyo imekuwa ikifanya kazi kubwa katika kusaidia viongozi kujifunza masuala ya uongozi wakiwemo viongozi wanawake kwa kuwapa nafasi ya kujifunza masuala ya uongozi.

Pia alisema takwimu bado zinaonesha kuwa kuna idadi ndogo ya wanawake katika nafasi za maamuzi hivyo kupitia mafunzo hayo yatasaidia kuongeza idadi ya viongozi na kufanana na kundi la wanaume katika nafasi za uamuzi.

Alisema amefurahishwa na ushiriki wa viongozi 28 kutoka Zanzibar katika mafunzo hayo ambao mwaka huu wameitika kwa wingi ukilinganisha na mwaka uliopita.

# Tanzania kimbilio matibabu nchi jirani

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, amesema Tanzania inapokea zaidi ya wagonjwa 5,000 kutoka nje ya nchi kila mwaka wanaokuja kupata matibabu na huduma za kibingwa.

Amesema hali hiyo inatokana na uwekezaji mkubwa uliofanywa na serikali kwenye sekta ya afya.

Aidha, kutokana na uwekezaji huo, amesema Wizara ya Afya imepunguza asilimia 97 ya wagonjwa kwenda nje ya nchi kwa ajili ya matibabu.

Dk. Mollel alisema hayo juzi alipokuwa akizungumza na watumishi wa afya wa Hospitali ya Rufani ya Benjamin Mkapa jijini hapa.

Alisema uwekezaji wa vifaa tiba vya kisasa na wataalamu unafanya Tanzania kuwa kimbilio la matibabu kwa baadhi ya nchi.

"Hii ni hatua nzuri kwetu sisi kwenye sekta afya,tunazisi kuitangaza Tanzania katika ubora wa utoaji huduma za afya. Si jambo dogo kabisa hivyo watumishi mnapaswa kuzidi kuweka jitihada za utoaji huduma bora hasa ukizingatia serikali imeboresha kwenye suala la vifaa tiba na miundombinu mbalimbali ya ujenzi katika hospitali zake," alisema.

Pia alisema tayari serikali imetia saini mikataba na Zambia na Malawi kwa ajili ya kuleta wagonjwa wao nchini kupata huduma za kibingwa na ubingwa bobezi.

"Serikali imetoa zaidi ya Sh. bilioni 51.4 katika hospitali za kanda ndani ya mwaka huu kwenye eneo la ujenzi na zaidi ya Sh. bilioni 290.9 zimetumika kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba katika hospitali za rufani za mikoa, kanda na taifa," alisema.

Alisema pamoja na serikali kufanya uwekezaji mkubwa katika sekta ya afya kwenye maeneo yote ikiwamo miundombinu, vifaa tiba na watumishi wenye ujuzi, kuna haja ya kusimamia ubora wa huduma ili wananchi wanufaike vyema.

Naibu Waziri huyo alisema watumishi wanapaswa kusimamia vifaa tiba pamoja na utoaji huduma stahiki kwa wagonjwa ili taifa liendelee kupata sifa nzuri kwenye huduma za matibabu ya kawaida,kibingwa na ubingwa bobezi.



Mkuu wa Wilaya ya Nachingwea, mkoani Lindi, Mohamed Moyo (mwenye kanzu), akipata maelezo wakati alipofanya ziara ya kukagua jengo jipya la wagonjwa mahututi (ICU), katika Hospitali ya wilaya hiyo juzi. Kulia ni Katibu Tawala wa Wilaya hiyo, Omari Mwanga. **PICHA: STEVEN WILLIAM.**

# Usafiri kikwazo mboga na matunda ughaibuni

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WADAU wa tasnia ya mazao ya bustani nchini, wamesema Tanzania bado inakabiliwa na tatizo la usafiri wa uhakika kwa ajili ya kusafirisha bidhaa zao nje ya nchi hali ambayo ni kikwazo kwa zile zinazoharibika haraka.

Meneja wa Mazingira ya Biashara wa Taasisi ya Wakulima wa Mboga na Matunda Tanzania (TAHA), Kelvin Remen, alisema hayo juzi kwenye mkutano wa wadau wa tasnia ya mazao ya bustani pamoja na uzinduzi wa Mwongozo wa Zao la Parachichi.

Remen alisema pamoja na jitihada mbalimbali zinazofanywa na serikali, Tanzania bado inakabiliwa na kero mbalimbali katika usafirishaji wa mazao ya bustani nje ya nchi.

Alisema kutokana na hali hiyo bidhaa za mazao ya bustani ambazo zimekuwa zikisafirishwa zimekuwa zikiharibika zikiwa njiani kabla ya kuwafikia walaji.

"Tanzania hatuna ndege za mizigo kwa ajili ya kusafirisha mazao haya ya bustani, hivyo kutumia ndege za abiria hali inayofanya kusafirisha nje ya nchi kiasi kidogo cha bidhaa hizo.

Tatizo lingine ni muda unaotumiwa katika viwanja vyetu vya ndege ni mkubwa hali ambayo inaweza kusababisha baadhi ya bidhaa kama nyanya kuharibika njiani.

"Sisi hapa tunazo ndege 14 za abiri wakati wenzetu Kenya wanazo zaidi ya 40 na Afrika Kusini wanazo zaidi ya 70, hivyo hatuwezi kushindana nao katika kusafirisha bidhaa hizo za mboga na matunda," alisema.

Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alisema serikali iko tayari kushirikiana na wadau hao kuendeleza tasnia hiyo ili kukuza uchumi wa wananchi.

"Njooni na mpango wa muda mrefu. Lazima tufahamu tunazalisha wapi tunauza wapi lakini jitihada zinazofanywa na serikali yetu ni kuhakikisha mazao haya yanasafirishwa na kuuzwa kwa wingi nje ya nchi ili kukuza uchumi wetu," alisema.

Aidha, Bashe alisema miradi mingi ya kilimo ambayo imekuwa ikianzishwa nchini kwa ufadhili wa wadau kutoka nje ya nchi imekuwa ikifa mara tuu wanapoondoka.

"Miradi mingi hata hii ya kilimo unakuta inafanya vizuri sana wanapokuwapo wafadhili lakini mara tu baada ya wahisani kuondoa inakufa, hivyo hakikisheni miradi yote inakuwa endelevu," alisisitza.

## Mil. 380/- kumaliza kero ya maji Handeni

**Na Beatrice Shayo**

ZAIDI ya wananchi 2,000 wa Kata ya Kideleko, Handeni mkoani Tanga wanatarajia kufaidika na mradi wa maji uliogharimu Sh. milioni 380 baada ya kukabiliwa na changamoto hiyo kwa muda mrefu.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi, Msimamizi wa Mradi wa Bwawa la Kwamaizi, Mhandisi Ulenaula Mwasimba, alisema mpaka sasa mradi umefikia asilimia 78.

"Litakuwa na chemba ya kutolea maji zitakazodhibiti bwawa hilo, hadi sasa imefikia asilimia 100. Kuna ujenzi wa tangi lililofikia asilimia 100 na tutaweka nyumba ya pampu ambayo sasa imefikia asilimia 70," alisema.

Justine Kimea, mkazi wa kijiji hicho, ameishukuru serikali na wafadhili kwa kuwajengea bwawa hilo litaondoa adha ya muda mrefu ya maji kijijini hapo.

"Tunashukuru kwa ujenzi huu kwa sababu mradi ulikuwa umechukua muda mrefu. Tunaweza kukaa hata miezi miwili hadi mitatu hatujapata maji. Tunaishukuru serikali na wafadhili kwa mradi huu," alisema.

Meneja Uhusiano wa Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL) inayofadhili mradi huo, Risper Hatibu, alisema wanatekeleza programu ya Water for Life iliyoanza mwaka 2018 na hadi sasa wamewekeza miradi 24 ya maji nchi nzima.

"Bia moja tunatumia maji mengi kuitengeneza, tukasema tutafanyaje ili kulinda maji? Ndiyo maana tumekuja na miradi hii ili kuhakikisha kunakuwa na upatikanaji endelevu wa maji," alisema.

Mkuu wa Miradi wa WaterAid, Happiness Willbroad, alisema ili kuweka uendelevu wa bwawa hilo wamechagua wanawake 24 na kuwapa mafunzo yakiwamo ya utunzani wa mazingira.

"Kazi yao ni kulitunza ikiwa pamoja na kuhakikisha mazingira yanayolizunguka yanaoteshwa miti. Mkuu wa Wilaya amesema tuweke samaki ambao baada ya miezi sita watavuliwa. Wanawake hawa watafanya kazi kwa kushirikiana na ofisi ya mtaa na Wilaya ya Handeni," alisema.

Willbroad alisema SBL imewapatia Sh. milioni 25 ambazo zimetumika katika kutoa mafunzo kwa wajasiriamali hao ili wajikwamue kiuchumi.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kauli ya Waziri Simbachawene ni somo kwa viongozi wanawake

**TAASISI** ya Uongozi juzi ilifanya mahafali ya programu za uongozi ambazo lengo lake ni kuwawezesha viongozi kuwa chachu ya maendeleo kuanzia ngazi za chini hadi taifa. Miongoni mwa wahitimu katika mahafali hayo yaliyofanyika ni wanawake ambao miongoni mwao ni watumishi wa serikali katika taasisi mbalimbali.

Wanawake wanapewa kipaumbele katika mafunzo hayo kutokana na wimbi la mabadiliko ya uwezeshaji wa jinsia hiyo katika uongozi na kuwamo katika ngazi za uamuzi. Shabaha ya kundi hilo kupewa nafasi ni kufikia uwiano wa 50 kwa 50 baina yao na wanaume kwenye ngazi za uongozi wa kitaasisi, kisiasa na ngazi za uamuzi kwa ujumla.

Kwa muda mrefu wanawake wamekuwa wachache katika nafasi za uongozi na uamuzi kutokana na sababu mbalimbali zikiwamo elimu, kipato na mfumo dume ambao umekuwapo kizazi hadi kizazi. Lakini kutokana na wimbi la mageuzi duniani Pamoja na haki za binadamu, wanawake wamekuwa wakiwezeshwa katika elimu na nafasi za uongozi na imani iliyojengeka imesababisha kuwapo kwa msemo kwamba wanawake wakiwezeshwa wanaweza.

Tangu kuwapo kwa wimbi hilo hususan baada ya Azimio la Beijing la mwaka 1995, kumekuwa na kasi kubwa ya wanawake kuingia katika uongozi na vyombo vya uamuzi katika maeneo mbalimbali ikiwamo mihimili ya dola, yaani Bunge, Serikali na Mahakama. Pia kumekuwa na mwamko mkubwa wa wasichana na watoto wa kike katika elimu na idadi kubwa ya wanaohitimu katika taasisi za elimu ya juu ni kundi hilo.

Kadhalika kumekuwa na wimbi kubwa katika kuwawezesha wanawake kiuchumi kwa kupewa mikopo mbalimbali ambayo imewasaidia kujikwamua kiuchumi na hata wengine kuwa na ukwasi kuliko wanaume.

Katika mahafali hayo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene, aliwataka wahitimu na wanawake kwa ujumla watambue kuwa uwezeshwaji kielimu na kiuchumi na kupewa nafasi za uongozi isiwe sababu ya kuibua jeuri na majivuno hasa wanapopanda vyeo au kuongezeka kwa kipato.


Simbachawene alisema lengo la serikali ni kuwa na viongozi watakaokuwa chachu ya maendeleo kuanzia ngazi ya familia mpaka taifa, hivyo wanawake kuwezeshwa kielimu na kiuchumi isiwe sababu ya kuinua mabega na kujenga kiburi na majivuno. Aliwasihi kwamba wanaporejea kazini wasiwe na tabia hizo hasa wanapopanda vyeo na kuongezeka kwa kipato huku akisisitiza kuwa iwapo wataendekeza tabia hizo wataharibu jitihada za serikali za kuwawezesha na kuwamo kwa wingi katika vyombo vya uamuzi.

Kauli hiyo ya Waziri Simbachawene imekuja kwa wakati mwafaka. Kama ni kisu basi kimegonga mfupa kwa sababu mambo aliyoyasema yanawagusa baadhi yao moja kwa moja kutokana na kasumba ya kujiona wako juu pindi wanapokuwa na madaraka.

Kumekuwa na baadhi ya kesi kwamba wanawake wanapokuwa na kipato na vyeo, wamekuwa na tabia ya kuwa na jeuri, kiburi na majivuno hata kuwanyanyasa walioko chini yao. Baadhi yao wamekwenda mbali zaidi kuwanyanyasa hata wenza wao na hata kuwakimbia kwa sababu wana madaraka na ukwasi kulinganisha na waume zao.

Elimu, vyeo na ukwasi wanavyopata visiwe fimbo ya kupigia wengine bali waonyeshe kuwa mfano katika nafasi za uongozi wanazopewa kuwa wanaweza na wanakuwa na upendo na moyo wa huruma. Pia waonyeshe kwamba wao ni chachu katika kuleta tija na ufanisi kwenye taasisi na taifa kwa ujumla.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Barabara ya Kilolo hadi Ipogolo itakamilika lini?

Na Sabato Kasika

**WILAYA** ya Kilolo ilianzishwa mwaka 2002 baada ya kugawanywa toka wilaya ya Iringa. Tangu mwaka 1961 hadi 2005, ilikuwa sehemu ya kata na tarafa za wilaya ya Iringa.

Pamoja na kuwa na umri wa zaidi ya miaka 20 sasa, Kilolo ni miongoni mwa wilaya zinazokabiliwa na vikwazo mbalimbali ikiwamo kutokuwa na barabara za kiwango cha lami inayounganisha makao makuu ya mkoa na wilaya.

Ingawa si wilaya ya kwanza kuwa na kikwazo hicho, kwa kuwa maelekezo yalishawahi kutolewa na Rais kwamba ijengwe kwa kiwango cha lami, nilidhani utekelezaji ungekuwa umefanyika.

Mei mwaka 2018, aliyekuwa Rais wa awamu ya tano, Hayati John Magufuli, aliagiza Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) na wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURAO kuanza mara moja ujenzi wa barabara hiyo yenye urefu wa kilomita 35 kwa kiwango cha lami.

Rais alitoa agizo hilo katika mkutano wa hadhara mjini Kilolo kwamba barabara hiyo kutoka mjini Kilolo ijengwe kwa kiwango hicho, ili kuondoa kero ya ubovu miundombinu ya wilayani humo Pamoja na sehemu ya wiaya ya Iringa kutoka Ndiwili hadi Ipogolo.

Hata hivyo, barabara hiyo imeendelea kubaki kama ilivyo, huku kilomita chache ndizo zikiwa zimejengwa kwa kiwango cha lami, kitendo kinachoonyesha huenda ujenzi ukachukua muda mrefu hadi kukamilika.

Kusuasua kwa ujenzi huo, kulishawahi kumfanya Mbunge wa Viti Maaluim Mkoa wa Iringa, Ritha Kabati, kuuliza swali bungeni akitaka kujua ni lini ujenzi huo utakamilika. Alijibiwa na aliyekuwa Waziri wa Nchi Ofsi ya Rais, Tawala za Miko ana Serikali za Mitaa (TAMISEMI), George Simbachawene (sasa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais-Utumishi) kwamba dhamira ya serikali ni kuhakikisha miundombinu ikiwamo ya barabara inajengwa.

Akaongeza kuwa hiyo inakwenda sambamba na ahadi zote za viongozi wakuu wa nchi na kumtaka mbunge huyo kuwapa muda ili watakapopata ratiba kamili ya suala hilo watalikeleza.

Vilevile kuna kilomita tano za lami eneo la makao makuu ya wilaya, kutoka kibaoni hadi Kilolo mjini, lakini pia kuanzia mwaka 2019 ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami ulianza kutoka Kibaoni hadi Ipogolo.

Lakini mwaka 2020 ulianzia Kibaoni kwenda mpakani mwa wilaya ya Kilolo na Iringa ikamilika kama kilomita mbili ambayo pia imeanza kubanduka, kitendo ambacho kinaweza kusababisha ujenzi ukarudiwa. Wakati lami hiyo ikibanduka, eneo la njiapanda hadi darajani, barabara ni mbovu, kwani wakati huu ambao mvua zinaendelea kunyesha, kuna mashimo, hivyo husababisha usumbufu kwa watumiaji wa barabara hiyo.

Kilolo imegawanyika katika tarafa tatu ambazo ni Kilolo yenyewe, Mazombe na Mahenge, ina kata 24 na vijiji 94, mitaa 16 katika mamlaka ya mji mdogo Ilula na vitongoji 499.

Aidha, Kilolo kama zilivyo wilaya zingine nchini, wakazi wake wanajishughulisha na kilimo cha mazao mbalimbali ya chakula na biashara yakiwamo mahindi, viazi na nyanya. Kwa sasa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI) imeanza kutekeleza mkakati wa kupanda miche ya parachichi kwa ajili ya kusambaza kwa wakulima wanaotaka kuwekeza kwenye zao hilo wilayani humo.

Kwa hiyo, ili wakulima wasafirishe mazao yao ya biashara kwenda sokoni, ni vyema wilaya hiyo iwe na barabara ya lami inayoinganisha na makao makuu ya mkoa na kisha kuunganisha kwenda mikoa mingine.

Kwa kuwa barabara hiyo ilipangwa kujengwa kutoa Kilolo hadi Ipogolo mjini Iringa, ninadhani itapndeza kama ujenzi wake utakamilika badala ya lami kuwa sehemu ndogo huku eneo kubwa likiachwa.

Ikumbukwe kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo ilishawahi kushika nafasi ya tatu katika maadhimisho ya Nanenane ya Nyanda za Juu Kusini yaliyofanyika mjini Mbeya mwaka 2017.

Halmashauri 39 zilishikiri kwenye maonyesho hayo huku Kilolo ikifanikiwa kunyakua nafasi ya tatu kikanda na nafasi ya kwanza kimkoa, hivyo ninadhani wakulima wake wangesaidiwa kuwa na barabara ya lami, ili warahusishe kusafirisha mazao yao.

## FIKRA MBADALA

# Wizara ya Elimu inastahili pongezi



Pascal Mayalla

**VETA ilipewa nafasi ya kipekee Aprili 25 ambayo iliitwa VETA Day. Siku hii ilitumika kutangaza shughuli zinazofanywa na VETA yikiwamo mafunzo yanayotolewa, ubunifu unaofanywa na walimu na wanafunzi, umahiri wa wanafunzi, bidhaa zinazozalishwa na kupitia vyuo vyake nchini kote na mafanikio ya wahitimu kwenye fani mbalimbali.**

LEO nazungumzia kitu kinachoitwa MAKISATU. Inawezekana hili ni neno jipya miongoni mwetu lakini ni kifupi cha Mashindano ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu, ambayo hufanyika kila mwaka.

Kilichofanyika kwenye mashindano ya mwaka huu, mtakubaliana na mimi kwamba waandalizi, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, kuanzia Waziri Profesa Adolph Mkenda, Katibu Mkuu Prof. Carolyne Nombo, Mkurugenzi wa Sayansi, Technolojia na Ubunifu, Prof. Maulilio Kipanyula, na timu yao yote ya wizara, idara, na taasisi zilizochini ya wizara hiyo, Mamlaka ya Ufundi Stadi (VETA), Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), Tume ya Nguvu za Atomiki (TAEC) na vyuo vikuu mbalimbali, wanastahili pongezi za dhati kwa kufanikisha jambo hilo kwa kiwango cha juu.

Kitu kikubwa zaidi ni kwa baadhi ya wabunifu wa Kitanzania, kuanza kubiasharisha ubunifu wao kwa kutengeneza bidhaa na kuziingiza sokoni, hivyo Tanzania kuanza kutumia baadhi ya bidhaa zilizobuniwa na Watanzania wenyewe. Kilichobaki ni uhamasishaji kwa Watanzania kupenda bidhaa za Kitanzania.

Tangu mwaka 2019, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kushirikiana na wadau imekuwa ikiendesha Wiki ya Ubunifu na Mashindano ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (MAKISATU) kwa lengo la kuimarisha mfumo wa ubunifu nchini. Wiki ya Ubunifu Tanzania ni sehemu ya mikakati ya serikali katika kuongeza hamasa kwenye matumizi ya sayansi, teknolojia na ubunifu kama nyenzo ya kuharakisha maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Wiki ya Ubunifu pamoja na mambo mengine, imekuwa ikiibua, kutambua na kuendeleza jitihada zinazofanywa na wabunifu na wagunduzi wa Kitanzania. Aidha, kupitia maadhimisho ya Wiki ya Ubunifu Kitaifa, watafiti, wabunifu na wagunduzi hupata fursa ya kuonyesha bidhaa zao, hivyo kujulikana na watumiaji wa bidhaa hizo.

**WIKI YA UBUNIFU 2023**

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia iliandaa Wiki ya Ubunifu Tanzania kwa mwaka 2023. Maadhimisho hayo yalihusisha pamoja na matukio mengine, mijadala mbalimbali na maonyesho ya ubunifu na teknolojia kutoka taasisi za elimu ya juu, taasisi za utafiti na maendeleo, mashirika na kampuni za umma na binafsi, VETA, TAEC, vyuo vikuu na shule za msingi na sekondari.

Vile vile, kumekuwa na siku maalum kwa ajili ya kuonyesha shughuli zinazofanywa na VETA na TAEC kwa lengo la kutoa elimu kuhusu shughuli za taasisi hizo kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Kaulimbiu ya Wiki ya Ubunifu kwa mwaka 2023 ilikuwa "Ubunifu kwa Uchumi Shindani".

**SIKU MAALUM YA VETA**

VETA ilipewa nafasi ya kipekee Aprili 25 ambayo iliitwa VETA Day. Siku hii ilitumika kutangaza shughuli zinazofanywa na VETA yikiwamo mafunzo yanayotolewa, ubunifu unaofanywa na walimu na wanafunzi, umahiri wa wanafunzi, bidhaa zinazozalishwa na kupitia vyuo vyake nchini kote na mafanikio ya wahitimu kwenye fani mbalimbali.

Mdahalo kwa njia ya mtandao kupitia ClubHouse ulioratibiwa na Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa, uliwashirikisha Watanzania dunia nzima.

Mdahalo huo wa wadau wa ufundi stadi ulikuwa na mada "Mchango wa Mafunzo ya Ufundi Stadi Katika Kuendeleza Ubunifu na Kuchangia Kusukuma Maendeleo ya Nchi Kiuchumi." Mdahalo ulifanyika kuanzia saa 12 jioni hadi saa 2.00 usiku.

Mawasilisho mbalimbali yametolewa kuhusu mafunzo ya ufundi stadi na fursa zake na wahitimu wa VETA walionyesha bidhaa zao na kitu kikubwa kuliko ni kushuhudia baadhi ya wahitimu kutoka vyuo vikuu nchini, baada ya kukosa ajira ya vitu walivyosomea, wakajiunga na VETA kusomea ufundi, na sasa wanaendesha maisha yao kwa elimu waliyoipata VETA na si elimu yao ya chuo kikuu.

SIKU MAALUM YA TAEC

Siku hii tulionyeshwa jinsi nguvu za atamiki zinavyosaidia kwenye tiba mbalimbali zikiwamo picha za X - Ray na vipimo vya CT Scan na MRI hadi jinsi tiba za viini tete, stem cell zinazovyotibu magonjwa sugu ambayo zamani yalikuwa hayatibiki. Tukutane wiki ijayo.

**Wasalaam**
**Paskali**
**0754270403**

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Wachekeshaji wanachekesha taaluma ya habari



Na Joseph Kulangwa (kulangwasos@gmail.com)

ZAMANI mtu ulipomaliza darasa la nne au la saba na ukashindwa kuendelea na sekondari, kazi za haraka zilikuwa za jeshi au ualimu.

Ndiyo sababu mzazi aliposikia mwanawe amefeli alipolalamika aliulizwa kwani kazi ya jeshi au ualimu hakuna!

Hivyo waliovuka hapo na kumaliza darasa la nane au zaidi ya hapo, ndio waliopata kazi nzuri za utawala na baadhi yao kuwa wahasibu wenye marupurupu makubwa.

Sifa za kuwa mwanajeshi zilikuwa urefu na uwezo wako wa kukimbia, haya mengine hayakuwa na ulazima ili mradi ulifika kufunzwa matumizi ya nguvu na silaha.

Ualimu, kwa kuwa ulishamaliza madarasa hayo, basi ni dhahiri mtu uliweza kuingia darasani kufundisha wale wasioyajua. Ndiyo sababu hata baadaye, tukawa na Sera ya Elimu kwa Wote (UPE).

Nakumbuka aliyemaliza darasa la saba chini ya UPE alifundisha elimu ya msingi tena kwa mafanikio makubwa tu. Mnakumbuka mliokuwapo miaka ya 1970, chini ya Azimio la Musoma.

Hata hivyo, dunia huenda ikibadilika, ndipo kuna wakati Rais Julius Nyerere, Rais wa Kwanza, alipotangaza kuwa hivi sasa tunataka kujenga jeshi dogo la kisasa. Msisitizo ukawa katika elimu.

Ndipo darasa la 12 ikawa sifa ya chini ya kuandikisha wanajeshi na kuachana na urefu na mbio. Jeshi likawa la wasomi na si la wenye maguvu.

Ualimu nao ukapanda hadhi, baada ya kuona UPE ilikuwa ikitupotezea wakati kwa kuzalisha vilaza badala ya wasomi, waliotakiwa kuendana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia.

Wakati huo fani zingine kama uanasheria, udaktari, uhandisi nakadhalika zikishikilia umahiri wa kisomi katika kupata wataalamu wao, tofauti na hizo mbili.

Baadaye fani ya uandishi wa habari nayo ikaibuka, hasa baada ya kuwapo vyombo kadhaa vya habari tofauti na vilivyomilikiwa na serikali na chama tawala.

Vikaibuka vyombo binafsi vilivyotakiwa kujitegemea na hasa kunyang'anyana watendaji na vyombo hivyo vikongwe, kwa kuzingatia kuwapo kwa vyuo vichache vya kufundishia wanahabari nchini.

Vyombo binafsi vikatumia nguvu ya fedha kurubuni na kuiba waliokuwa waandishi na watangazaji wa vyombo vya umma ili kujiimarisha. Vilifanikiwa sana na kuibuka vingi kama uyoga.

Hali hiyo au mazingira hayo yakasababisha upungufu wa waandishi na watangazaji kwa kuwa jiko la kuwapika halikutosha, vyuo havikutosha, hivyo wakaanza kuchukuliwa watu wanaojua kusoma na kuandika, hususan kwa vyombo vilivyotumia lugha ya Kiswahili. Hao wakajazana huko na kupigwa msasa kila fursa ilipopatikana.

Nakumbuka siku moja tukiwa katika chombo kimoja cha habari, tulimuudhi mkurugenzi wetu kwa kuchelewesha gazeti mtamboni, akatuibukia na kuhamaki: "Kama mnashindwa kuwahisha gazeti, basi mimi nitakwenda pale Kariakoo, nitaita nani anajua kusoma na kuandika hadithi (stori) watakuja na ninyi nitawafukuza."

Tulipomwambia tatizo la ukosefu wa stori, akatuona kama mazwazwa hivi, akicheka kwa kejeli, na kuhoji: "Kwa nini msichukue hadithi za gazeti la mchana (jina linahifadhiwa) mkahamishia kwenye hilo la jioni?"

Hatukumjibu, lakini tukaelewa katika dhana ya kuamini kwake kuwa uandishi wa habari hauhitaji usomi, bali kama unajua tu kuandika 'mama analima au baba anasoma au kaka anakula na dada anafua', basi unaweza kuandika habari!

Ndiyo hayo tunayokumbatia hivi sasa, yaliyosemwa hivi karibuni na mwanahabari mwandamizi, Zamaradi Kawawa, kuhusu wachekeshaji waliochomekwa kwenye vyombo vya habari kama watangazaji.

Kwamba kwa kuwa unaweza kuchekesha mitaani, basi unaweza kutangaza redioni au luningani na ukaelewesha watu. Hiyo ni kutokubaliana kuwa dhima ya msingi ya chombo cha habari ni kuarifu, kuelimisha na kuburudisha.

Zamaradi akashauri watu hawa wakasomee taaluma hiyo, kwa sababu wanakengeuka misingi yake, wanajiweka katika uchekeshaji muda wote, na kusahau kuwa hiyo ni taaluma.

Utawasikia wengine wakiporomosha matusi, wengine wakipiga mikelele, wengine ndiyo kwanza wakisimama na kurukaruka studio.

Mbaya zaidi, hata staili ya kuhoji mtoa habari hawaijui na matokeo yake wanajisahau na wengine kuomba ofa hususan wanapokuwa wamealika mgeni mwenye kampuni ya uzalishaji bidhaa, ambaye hujikuta ameombwa hata ofa ya godoro au simu.

Baadhi yao ni wanaotumia fursa hiyo kuimba mapambio kwa wanasiasa, wakiwatukuza na kuwapigia wanayoita kiki huku wakijitambulisha kwa uchawa.

Hivi mchekeshaji anaweza kuingia thieta kupasua mgonjwa bila mafunzo ya utabibu? Mchekeshaji anaweza kuingia mahakamani kuwakilisha mshtakiwa bila kwenda Shule Kuu ya Sheria? Anaweza kusanifu ujenzi wa barabara bila kusomea uhandisi? Tasnia inabakwa, inanajisiwa kweupe. Hatua ichukuliwe.

**Alamsiki!**

# Tanzania inavyoweza kunufaika na utafiti anga nje

**Na Mwandishi Wetu**

HISTORIA inaonyesha kuwa siku moja binadamu alimudu kupanua wigo wa uwezo wake, hivyo kuthibitisha kwamba ushirikiano na sayansi vinaweza kubadilisha maisha ya kila mtu.

Moja ya siku hizo ilikuwa Aprili 12, 1961 baada ya raia wa uliokuwa Umoja wa Kisoveti wa Urusi (USSR), sasa Russia, Yuri Gagarin, aliruka angani nje kwa chombo chake akiwa binadamu wa kwanza aliyetoka angahewa.


Mwanzoni mwa safari yake alitamka mwito wake maarufu "Twende!", neno lililo kawaida kabisa katika maisha ya kila siku ya mwanadamu, bali lenye maana kubwa katika muktadha wa historia. Alifanya mzingo mmoja wa dunia na baada ya safari yake kukamilika, binadamu wote walijionea kuwa dunia kama mchanga mdogo katika ulimwengu usio na vikomo na ndio mwujiza wa kweli kwamba tupo hapa tulipo.

Wakati huo USSR kama ilivyo Russia kwa sasa, ilikuwa katika mstari wa mbele wa kufanya utafiti wa anga nje. Kabla ya safari ya mtu wa kwanza angani mwaka 1957, Urusi ilirusha satelaiti bandia ya kwanza pasipo mtu.

Kilichoiwezesha nchi hiyo ifikie mafanikio kama hayo ni sayansi, utafiti na viwanda na vyote hivyo vilichukua miongo mingi.

Aliyekuwa mwanamke wa kwanza angani nje ni Valentina Tereshkova (ambaye ni mbunge katika Bunge la Russia). Mtu wa kwanza aliyetoka nje ya chombo chake kwenda giza la anga nje alikuwa Alexey Leonov. Orodha hii ya mafanikio ya nchi hiyo ni ndefu sana wakiwamo waliorusha vyombo vya kwanza vya kuchunguza mwezi na sayari ya Venus.

Wakati huo Marekani pia ilifikia mafanikio makubwa katika fani hiyo. Walioacha nyayo za kwanza za binadamu mwezini ni Wamarekani. Vilevile wanajulikana kwa kutengeneza na kurusha vyombo vyao pasipo mtu vilivyofikia sayari za mbali za mfumo wa jua letu. Hivi karibuni nchi kadhaa za Ulaya, China na India ziliimarisha uwezo wao wa kuchunguza anga nje.



Setelaiti ikiwa katika anga nje. Pichani chini, mwanaanga wa Marekani akiwa katika anga za juu.



Ni dhahiri kwamba hivi sasa utafiti wa anga nje hauwezekani bila ushirikiano madhubuti wa kimataifa. Leo, wakati safari za anga nje zimekuwa jambo la kawaida, mataifa 14 yanashirikiana kupitia programu ya Kituo cha Kimataifa cha Anga Nje kinachoruka kilomita 400 juu na nchi nyingi za Asia na Afrika zinaonyesha hamu ya kushiriki katika kazi yake.

**MANUFAA KWA TANZANIA**

Matunda ya kivitendo ya taaluma za anga nje kwa sasa nchi zinayoyapata, yanathibitisha umuhimu wa Tanzania kushiriki katika uchunguzi wa anga nje. Hata satelaiti moja inaweza kuisaidia nchi katika sekta mbalimbali za kiuchumi zikiwamo kilimo, utalii, uchimbaji wa madini, matibabu na mawasiliano.

Akiwa kwenye anga nje, mwanaanga anaweza kukiangalia kilimo kinavyokua na kutafuta ardhi nzuri kwa mazao mbalimbali.

Kwa njia ile ile, mwanaanga anaweza kutafuta mahali penye madini kwa kuchunguza uwanda (landscape) wa nchi. Jinsi hiyo ya utafutaji wa madini, inatoa msukumo wa maendeleo kwa sekta ya madini na kwa jumla maendeleo ya kiuchumi.

Sekta ya utalii, hususani hifadhi kubwa za taifa, satelaiti zilizoko angani nje zitasaidia kuwaangalia wanyama porini na njia wanavyohama. Mtu ataweza kuangalia maisha ya kila mnyama na wataalamu wangeweza kupata habari muhimu za kufaa juu ya wanyamaporini ili kuuwezesha usitawi wa mazingira kwa wanyama.

Mawasiliano ni sekta nyingine ambayo mtu ana nafasi ya kutumia matunda ya taaluma za anga nje kwa sababu hivi sasa idadi kubwa ya watu wana simu za mkononi za kileo ambazo zina ramani za kidijitali tunazozitumia tunapotafuta mahali popote. Hivyo satelaiti inaweza kuyaboresha mawasiliano ya simu na hali ya 'navigation' ya simu ya mkononi.

Kwa mantiki hiyo, taaluma za anga nje na habari kutoka satelaiti zinatumiwa katika kila sehemu ya maisha yakiwemo matibabu kwa kuwa angani nje kunaendeshwa majaribio ya tiba ambayo matokeo yake yanatiliwa maanani na watu duniani.

Wakati wa kujadili suala la matazamio ya Tanzania ya kushiriki katika uchunguzi wa anga nje umewadia.

Sababu ni kwamba uchunguzi wa anga nje ni nafasi mwafaka inayoweza kutumiwa kwa maslahi ya ukuaji wa kiuchumi na kwa manufaa ya umma.

Nchi za Afrika zikiwamo Zimbabwe, Uganda, Angola, Kenya na Ghana zimeshazipeleka satelaiti zao katika anga nje zikatumia habari kutoka satelaiti zao katika elimu ya urasimu wa ramani, upimaji ardhi, utafutaji wa maeneo ya kuchimba madini na utengenezaji wa mtandao wa mawasiliano ya simu.

Kauli kama hizi zimeelezwa pia hivi karibuni na mwanaanga wa Russia, Sergei Kud-Sverchkov aliyekuwa ziarani Tanzania akakutana na wanafunzi, waandishi wa habari na raia wa kawaida Dar es Salaam.

Akisimulia safari yake angani nje alieleza pia juu ya mashirika yahusikayo na shughuli za anga nje likiwemo shirika la Roskosmos linalojishughulisha na mambo ya anga nje la Russia.

Roskosmos inazisaidia nchi nyingi zikiwamo za Afrika katika utengenezaji na ujenzi wa satelaiti na pia linawafundisha wanafunzi wageni kufanya kazi katika fani ya anga nje. Kwa mantiki hiyo, wakati umewadia kwa Tanzania kuchukua hatua ya dhati katika uchunguzi wa anga nje.





Wanaanga wa Russia, Yuri Gagarin (kushoto) na Sergei Kud-Sverchkov, wakiwa angani nje nyakati tofauti. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

# MAISHA

MEI 7, 2023
Nipashe
Baba, Mama na Mwana
Jumapili



Ukurasa 14


## JUISI YA TANGAWIZI

## MAISHA NI NYUMBA



Ukurasa 15

Hakikisha nyumba yako inapitisha hewa ya kutosha




## KATUNIKA


Ukurasa 16




## Mafuta ya nazi yanavyonogesha urembo

Ukurasa 14


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA






| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| P | ■ | C | H | O | T | A |
| A | ■ | ■ | ■ | B | ■ | S |
| M | ■ | K | A | A | ■ | H |
| B | U | U | ■ | M | T | I |
| A | ■ | M | B | A | ■ | N |
| N | ■ | B | ■ | ■ | ■ | D |
| A | W | E | K | E | ■ | E |


## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:

MTI, OFA, MFU, TIN, WANGA, ASALI, MAMBA, NYUTI, AMINIKA, NYOOSHA

## TOA TOFAUTI 5



## AMSHA AKILI

WIKI HII TUNACHEMSHA AKILI KWA NAMBA. TAFUTA VIFUNGU VIFUATAVYO VYA NAMBA KATIKA JEDWARI HAPA CHINI. VIFUNGU HIVYO VIPO KUTOKA KUSHOTO KWENDA KULIA NA JUU KWENDA CHINI

**1942, 559, 6354, 9428 na 3288**

176354847623
173687483492
945839428578
485938953848
209428948429

## WATOTO

# PAKA RANGI




## CHEKA

MZUNGU mmoja alionekana kumdharau Mbongo, akamwambia waulizane maswali na akishindwa anampatia Sh. 5000 na endapo yeye atashindwa atatoa 100,000.

**Mzungu:** Nchi ipi ilishindwa kwenye vita kuu ya kwanza ya Dunia?

**Mbongo:** akashindwa akatoa 5000 kuashiria hajui.

**Mbongo:** Kitu gani kikienda juu kina miguu minne na kikirudi chini kina miguu mitatu?

**Mzungu:** akafikiria akakosa jibu akatoa 100, 000, kuashiria hajui ila akataka kujua, akauliza ni nini hicho?

**Mbongo:** Akatoa 5000 kuashiria hata yeye hajui!.

**SWALI**

Samaki aina ya Pweza ana mikia mingapi?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Aliondoka ana mimba ya mtu mwingine, sasa anataka arudi!

KARIBU tena msomaji wangu tujadili misukosuko inayotesa familia zetu kila uchao. Vituko havikosekani katika kila nyumba unayoiona yenye baba, mama na watoto. Viko vituko vinavyofanana na vingine kutofautiana kulingana na tabia za wahusika.

Hebu sikia kituko hiki ikiwa ni mwendelezo mjadala wa ile roho ya ujinga inayotesa watu kama ilivyojitokeza katika makala kadhaa zilizopita ndani ya safu hii ya Maisha Ndivyo Yalivyo!

Msomaji wetu mmoja mapema wiki hii alituma ujumbe kuomba ushauri wa yale anayopitia katika familia yake. Akasema hivi;-

“Mke wangu tuliachana miezi minane iliyopita. Lakini wiki moja iliyopita akanipigia simu akiomba msamaha turudiane. Ila nimegundua kuwa ana ujauzito mimba miezi mitatu ya mtu mwingine. Mke huyu nilishazaa naye watoto wawili. Naomba ushauri nifanyeje?

Msomaji huyu baada ya kunitumia ujumbe huu, ilibidi nimpigie simu kupata maelezo ya ufafanuzi zaidi ikiwa ni pamoja na mazingira ya kuondoka nyumbani mkewe.

Akasimulia kwamba, mke wake walikuwa wakiishi vizuri wilayani Kahama na hawakuwahi kuwa na ugomvi wowote. Amezaa naye watoto wawili, wa kiume na kike, mmoja akiwa na umri miaka mitano mwingine miaka mitatu.

Mwanamke huyu kwao ni wilayani Geita. Mazingira ya kuondoka ni kwamba mama mkwe alituma taarifa kwamba anaumwa na alitaka binti yake aende kumuuguza. Mwanaume akaridhia akaondoka na watoto.

“Nikawa nawasiliana naye kwa simu kujua hali ya mgonjwa inavyoendelea na watoto. Ilipofika miezi miwili nikamwambia sasa inatosha arudi nyumbani Kahama kwani huko walikuwepo pia ndugu wengine wa kumhudumia mgonjwa.

Akasema hawezi kuja kwani mama yake bado hayupo sawa. Pia akanishawishi eti nitoke Kahama nihamie kabisa hapo nyumbani kwao. Nikashangaa sana! Si nitakuwa mimi nimeolewa kwenda kuishi na mke wangu kwa wakwe?

Baada ya miezi minne ilibidi nifunge safari kumfuate niweze kujua ukweli ya kile kinachoendelea. Kufika nikakuta wote hawajambo na hata mama yake alikuwa anafurahi na wajukuu zake.

Nikiwa pale katika kumchunguza nikagundua kama ni mjamzito. Ilibidi nikae naye pembeni nimhoji kulikoni mbona kama mjamzito vile! Nilipombana sana akakiri ni kweli.

Nikamuuliza mimba ya nani akasema ni ya jamaa wa hapo kijijini kwao. Akataka nimsamehe eti ibilisi alimpitia akaruhusu mahusiano na mtu mwingine japokuwa ni mke wa mtu.

Nilifadhaika sana. Akaniomba msamaha eti aweze kurudi nyumbani Kahama. Nikamwambia haitawezekana kwani tayari ana mimba ya mtu mwingine na siwezi kuilea mimba hiyo wakati mwenyewe yupo!

Pia ni kitendo cha dharau na aibu kwangu mbele ya jamii inayonizunguka. Ndugu, jamaa na marafiki zangu wataniona kituko kuishi na mwanamke mwenye mimba ya mtu mwingine.

Mpenzi msomaji, tulipofikia katika hatua hiyo ya mazungumzo, nikamuuliza kijana huyu ambaye umri wake ni miaka 28 kwamba yeye binafsi, ndani yake ana maamuzi gani baada ya hayo yote?

Akasema hivi: “Mimi ni mkulima hapa kwetu Kahama. Nimeona huyo mwanamke aendelee na huyo aliyempa mimba kutokana na kutokuwa mwaminifu.

Pia ili watoto wangu watulie wabakie hapo kwa bibi yao wasoma na tayari huyo mkubwa ameandikishwa darasa la kwanza. Mimi nitatuma fedha kuwahudumia pamoja na ada zao na pia nitakuwa nawatembelea kila inapopatikana nafasi.”

Mpenzi msomaji, hayo ndiyo yaliyomkuta kijana huyo aitwaye Shija sanane, ambaye ni mfuatiliaji mzuri wa safu hii. Aliona isiwe shida kwani bado ana nguvu za kufanya kazi asomeshe watoto wake na umri wake pia unamruhusu kutulia na kumuomba Mungu amchagulie mke mwingine atakayeishi naye. Ama kweli Maisha Ndivyo yalivyo!

Kitu cha kujiuliza hapa ni kwamba kama wawili hawa hawakuwa na ugomvi ni kitu gani kilichofanya binti yule kuamua kuwa na mahusiano na mtu mwingine huku akijua ni mke wa watoto wawili?

Alipobanwa na mumewe ataje mwanaume mwenye ule ujauzito alifanya hivyo, huku akidai ibilisi ndiye aliyemdanganya. Inawezekana ni kweli ibilisi kwani hutumia mbinu mbalimbali kuharibu hatma ya mtu.

Pengine pia yule mwanaume aliyempa mwanamke huyu ujauzito alikuwa rafiki yake wa zamani hapo kijijini. Sasa walipokutana wakakumbuka maisha ya zamani, yakatokea hayo.

***Je, una kisa au ushauri? Ujumbe 0715268581.***

## WARAKA WA NDANI

Na Godfrey Mushi



# Kupuuza tathimini ya athari za mazingira hakutuachi salama

TATHMINI ya athari za mazingira (EIA) inayotakiwa kufanywa kisheria na maofisa wa Baraza la Taifa la Usimamizi na Uhifadhi wa Mazingira (NEMC) ni mchakato wa kutathmini na kupunguza athari za ‘biophysical’, kijamii na zingine zinazofaa za mapendekezo ya maendeleo, kabla ya uamuzi kuchukuliwa.

Kwa wale ambao hatujafuatilia mambo haya ni kwamba tathmini ya athari za kimazingira hutumiwa mara kwa mara kwa kuwa ina manufaa zaidi katika taifa lolote lile duniani. Nchi haiwezi kuwa na seti ya sheria na kanuni zilizoendelezwa vizuri ambazo hazifanani kwa uwazi au kulazimisha ni shughuli zipi na mambo yapi yanaweza kuruhusiwa.

Kama ndivyo! kuna hatua kadhaa muhimu ambazo kwa ujumla hufuatwa katika mchakato wa tathmini ya athari za mazingira ambazo ni uchunguzi na upimaji, tathmini ya hatari ya mazingira, ushiriki wa wadau, udhibiti wa mpango na kufanya uamuzi.

Nimeguswa kuanza na mwongozo huo wa hatua za kitaalam kutokana jicho la ziada la Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Charles Kichere, katika ukaguzi wake alioufanya, na kuweka mapendekezo yake kwenye Ripoti ya Mwaka ya Ukaguzi wa Ufanisi ya Mwaka 2021/22.

Ni makosa makubwa kutotazamwa hatari kwa makazi, kubeba uwezo wa mradi na kujumuisha mahitaji ya tathmini ya msingi; kwa sababu ripoti ya EIA kwa kawaida huwa na tathmini ya njia mbadala zinazopendekezwa katika mradi.

Katika ripoti hiyo, CAG amebaini pamoja na mambo mengine, utekelezaji wa miradi ya ujenzi yenye thamani ya Sh. bilioni 23.80 kufanyika bila tathmini ya athari za mazingira.

Kanuni ya 241 (3) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013, inazitaka taasisi zinazofanya ununuzi kufanya tathmini ya athari za kimazingira katika hatua ya maandalizi ya mradi, kabla ya kuanza mchakato wa ununuzi.

Aidha, Kifungu cha 81 (2) cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura ya 191, kinataka utafiti wa tathmini ya athari za mazingira ufanyike kabla ya kuanza au kufadhili mradi.

Kwa matakwa ya sheria na kanuni hizo, CAG anasema amepitia majalada ya miradi na kubaini kuwa mamlaka 12 nchini zilianza utekelezaji wa miradi yenye thamani ya Sh. bilioni 23.80, bila kufanya tathmini ya athari za mazingira kabla ya kuanza miradi hiyo.

Aidha, CAG anasema amebaini kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Rombo, inatekeleza mradi wa ujenzi wenye thamani ya Sh. bilioni 2.80 bila kufanyika uchunguzi wa kijiolojia.

Kwa mujibu wa CAG, miradi hiyo iliyotekelezwa bila tathimini ya athari za mazingira ni ya Halmashauri ya Wilaya ya Bunda iiliyotumia Sh. 3,578,773,698, Halmashauri ya Singida Sh. 3,459,892,600, Halmashauri ya Jiji Dar es Salaam (wakati huo) Sh. 2,930,234,090.

Kuna Halmashauri ya Wilaya ya Rombo Sh. 2,800,000,000, Bumbuli Sh. 1,000,000,000, Halmashauri ya Wilaya ya Monduli Sh. 2,500,000,000, Halmashauri ya Mji Geita Sh. 2,407,569,051.

Zingine ni Halmashauri ya Muheza Sh. 1,500,000,000, Halmashauri ya Mji Singida Sh. 1,470,000,000, Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto Sh. 1,150,000,000, Halmashauri ya Siha Sh. 500,000,000 na Halmashauri ya Wilaya ya Songea Sh. 500,000,000.

CAG anasema kimsingi utekelezaji wa miradi, bila kufanya tathmini ya athari za mazingira na uchunguzi wa kijiolojia, unaziweka mamlaka za serikali za mitaa

katika hatari za kupata athari za mazingira, ambazo zinaweza kuathiri jamii katika maeneo husika, na kusababisha hasara ya upotevu wa rasilimali.

Na kutokana na udhaifu huo, ameshauri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), ihakikishe Mamlaka za Serikali za Mitaa, zinafanya tathmini ya athari za mazingira na uchunguzi wa kijiolojia, kabla ya kuanza kwa mradi wa ujenzi ili kuhakikisha unakuwa salama.

Godfrey Mushi, ni Mwandishi Mwandamizi wa Nipashe, Kanda ya Kaskazini. **Anapatikana kwa simu namba 0715 545 490 au barua pepe: ghandsome79@gmail.com**

# HARUSI







ILIKUWA SIKU YA FURAHA KWA BWANA GAUDIN GRATION ALIPOFUNGA NDOA TAKATIFU NA BIBI ANA DEUS DESEMBA 30, 2022, KATIKA KANISA KATOLIKI LA KATOKE WILAYANI MULEBA MKOANI KAGERA NA BAADAE KUFUATIWA NA TAFRIJA FUPI ILIYOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA SUZANA.





# MITINDO

Na Mary Geofrey

## Vazi la Abaya na umaarufu wake

SIKU hizi ni nadra sana kutokutana na binti au mwanamke aliyevaa vazi la abaya ambalo limejizolea umaarufu.

Uvaaji wa vazi hili sio kwa Waislamu pekee, bali hata kwa watu wa dini nyingine wanaowaunga mkono marafiki zao wa dini hiyo.

Wakati wa msimu wa mwezi Mtukufu wa Ramadhani vazi hili lilishika kasi kutokana wanawake wengi kujisitiri.

Mavazi kama baibui, madera, magauni marefu ya kanga, vitenge, batiki, kaniki yamemezwa na vazi hili la abaya.

Vazi hili limepata umaarufu katika siku za usoni kutokana na kuboreshwa katika mitindo mbalimbali ya kisasa.

Kwa sasa vazi hili linaboreshwa kwa kuwekewa nakshi, jambo linalofanya watu kuendelea kulivaa na kupata umaarufu.

Abaya ni vazi jeusi au rangi yoyote ya kung'aa linalofanana na baibui, linalo valiwa juu ya nguo ambalo asili yake ni nchi za Uarabuni kama vile Dubai, Oman, Saudia na nchi za Uturuki, Indonesia, India, Pakistan na nyinginezo.

Vazi hili limekuwa tishio kutokana na kuuzwa bei kubwa tofauti na baibui na mavazi mengine ya stara.

Wavaaji wa vazi la abaya wamekuwa wakivutia watazamaji kutokana na kuwa linatulia mwilini na linaloweza kuvaliwa na mtandio unaofanania na rangi ya gauni hilo au kuchanganya rangi ambazo zinaleta mvuto.

Kama ambavyo unaona kwenye picha vazi la abaya linavyovutia nawe unaweza kulivaa ili kwenda na mtindo mpya wa mavazi unaoendelea ndani na nje ya nchi.







UREMBO

**Na Mary Geofrey**



# Mafuta ya nazi yanavyonogesha urembo

MAFUTA ya nazi yamekuwa yakitumika kupaka mwilini, kwenye nywele na kufanya masaji.

Mbali na kazi hizo mafuta ya nazi yana matumizi mengine muhimu kwa ajili ya urembo wa ngozi na mwili.

**Make-Up Remover**

Mafuta ya nazi yanaweza kutumika kuondoa make-up usoni. Chukua pamba chovya kwenye mafuta ya nazi kisha tumia kusugua kwenye sehemu za uso ulizopaka make -up yako.

**Kusafisha uso**

Paka mafuta ya nazi sehemu z a shingoni na usoni kisha fanya masaji halafu jifute kwa kutumia kitambaa au taulo.

**Scrub mwili mzima**

Chukua vijiko vitano vikubwa vya sukari kisha changanya na vijiko vitano vikubwa vya mafuta ya nazi kisha koroga mchanganyiko wako halafu utumie kufanyia scrub.

**Scrub ya uso**

Changanya mafuta ya nazi na amira au makande pamoja na mdalasini kisha tumia kufanya scrub usoni .

**Kunyolea**

Jipake mafuta ya nazi katika sehemu yenye nywele kisha anza kunyoa.

**Kujipaka**

Unaweza kutumia mafuta ya nazi kujipaka.

Unaweza kuongeza na marashi ya rose ili kuyafanya mafuta yawe na harufu zzuri.Matumizi ya mafuta ya nazi mwilini huifanya ngozi yako kuwa na afya njema.

Kuondoa makunyanzi

Jipake mafuta ya nazi juu ya macho ili kuondoa makunyanzi.





MAPISHI

**Na Mary Geofrey**

# Juisi ya tangawizi, asali na faida lukuki

JUISI ya Tangawizi ni nzuri kwa matumizi ya binadamu na hasa iliyochanganywa na asali.

Juisi hii inatengenezwa kwa kutumia tangawizi nne kubwa, asali vijiko saba vya asali mbichi, parachichi moja, ndimu kidogo moja kama utapendelea na maji lita moja na nusu.

Ukishachanganya unasaga kwa pamoja na kuchuja na juisi yako itakuwa kwa ajili ya kunywa na chakula chochote.

Juisi hii ya tangawizi kwa mtu mzima unaweza kunywa glasi moja yenye ujazo wa robo lita mara mbili kwa siku (asubuhi na usiku) na mtoto wa miaka mitano mpaka 11 anaweza kunywa glasi moja mara moja kwa siku.

**Faida za juisi**

Huua bakteria wa aina nyingi mwilini hata Salmonella ndani ya mwili hata juu ya ngozi.

Tangawizi huua kimeng'enya ambacho ni chakula cha seli za kansa ya tezi dume na seli hizo za kansa hufa ndani ya saa mbili au nne bila hicho kimeng'enya.

Huondoa sumu mwilini haraka, uvimbe, homa ya baridi (chills), msongamano mapafuni na kuna viua vijasumu (antibiotics) vya asili viwili kwenye tangawizi.

Aidha, huondoa sumu mwilini haraka, maumivu ya koo, hutibu saratani ya tezi dume. Ni dawa nzuri kwa kansa ya kwenye damu (leukemia), huongeza msukumo wa damu na hutibu kansa zinazoweza kusababishwa na kupata choo kigumu muda mrefu.

Hupunguza mishtuko kwenye utumbo mpana na tumbo kuunguruma, husaidia kuzuia kutapika.

Husaidia hata wale wanaosafiri baharini wasipatwe na kichefuchefu, hutibu homa ya kichwa na huimarisha afya ya figo.

Hulinda kuta za moyo, hulinda mishipa ya damu na mishipa ambako mikojo hupita na madini ya manganese ambayo ni mhimu katika kuuongeza mfumo wa kinga ya mwili dhidi ya magonjwa mbalimbali.

Hutibu homa za asubuhi hata kwa mama mjamzito na husaidia mfumo wa upumuaji na kutuliza dalili za pumu.







MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya



# Hakikisha nyumba yako inapitisha hewa ya kutosha

NYUMBA bora ni ile iliyotengenezewa mifumo mizuri ya uingizaji wa hewa. Nyumba inapokosa mifumo mizuri ya kuingiza hewa, hapo ndipo na vichafua hewa ndani huanza kujijenga.

Changamoto kubwa iko zaidi kwenye nyumba za kisasa kutokana na nyingi kuzibwa kila mahali, jambo ambalo limeonekana kuwa la kawaida hasa milango na madirisha yanapokuwa yamefungwa kwa muda mrefu kuliko yanavyofunguliwa.

Njia rahisi ya kuondoa tatizo hili ni kufungua madirisha kila siku pamoja na kuhakikisha nyumba inafanyiwa usafi katika kila njia ambayo ni chanzo cha kuingiza hewa.

Jambo lingine ni kuzingatia usafi wa jumla wa nyumba nzima, kwamba sakafu ziwe safi na zisafishwe kila inapobidi.

Kutokuruhusu taka, nguo chafu, vumbi na uchafu mwingine kujijenga kwa sababu unakaribisha uwezekano wa kuharibu hali ya hewa ndani ya nyumba.

Kutoruhusu vyombo vichafu vijazane kwa muda mrefu bila kusafishwa na pia kuepuka kuhifadhi nguo chafu kwa muda mrefu bila kufuliwa na kufuta fumbi kila wakati.



Pia kama unavyo vifaa vya kisasa vihusianavyo na maboresho ya hewa ya ndani kama vile viyoyozi na feni, hakikisha vinafanyiwa usafi wa mara kwa mara ili machujio yake yasibebe vumbi na kushiriki kulisambaza.

Sababu nyingine inayochangia uwapo wa hewa nzito na chafu ndani ya nyumba ni uvutaji wa sigara ndani na ni jambo baya ambalo linapaswa kupigwa marufuku kwa kuwa pia linaleta hatari kubwa kiafya.

Hewa hiyo binadamu anahitaji aipate katika kila mahali anapokuwapo iwe ni sehamu pa kazi, nyumbani na kwingineko.

Hivyo basi kutokana na umuhimu huo wa hewa kwa binadamu, nyumbani napo ambapo ni mahali muhimu anapotumia muda wake mwingi panahitajika pawe na hewa ya kutosha, si tu hewa lakini pia iwe safi.

Wakati mwingine unaweza ukaingia ndani ya nyumba ukakutana na hewa nzito, ambayo ukikaa muda mfupi unahisi maumivu ya kichwa kwa mbali.

Binadamu tunatofautiana,wapo ambao wana uwezo mkubwa wa kuhisi kitu chochote ambacho hakiko sawa kwa haraka ndani ya nyumba hasa upande wa harufu au kunapokosekana hewa nzuri na safi.

Matatizo hayo ya uwapo wa hewa mbaya ndani ya nyumba yanaweza kuwasababishia wanafamilia matatizo ya kiafya endapo hakutakuwa na ufumbuzi wake au jitihada za kuweka mazingira ya nyumba kuingiza hewa safi.

Inawezekana mwanzoni likaonekana ni jambo gumu la kufanya, ila ni kwamba kuboresha hali ya hewa ya ndani ni rahisi sana, unachotakiwa ni kuzingatia tu mambo machache, na unaweza kuwa na nyumba huru isiyo na harufu na isiyokuwa na vichafua hali ya hewa.

## Zingatia haya kupendezesha nyumba yako

**Na Restuta James**

WATU wengi wanakabiliwa na tatizo la namna ya kupanga nyumba kwa sababu ya kutozingatia vitu vidogo vichache, ambavyo vinaweza kuwafanya waifurahie sebule au chumba cha kulala.

Anza na panapookenaka

Kabla hujaanza kupanga kitu chochote katika sebule au chumba chako ni muhimu sana kuzingatia sehemu ambayo macho 'yanapiga' zaidi ili uweke kitu kitakachokufanya ufurahie unapoingia nyumbani kwako.

Eneo hili linaweza kujitengeneza lenyewe mathalani dirisha kubwa au usanifu mwingine wowote uliofanyika wakati wa ujenzi. Vinginevyo unaweza kulitengeneza kwa mfano eneo ambalo luninga na miziki vitakaa.

Usigusishe kochi na ukuta

Ukubwa wa chumba au sebule, ndio unaamua ni eneo kiasi gani libaki ukutani bila kugusana na fenicha, ingawa hata kwenye sebule ndogo kabisa unapaswa kuacha.

Acha nchi kadhaa kati ya migongo ya fenicha na ukuta. Lakini kama una chumba kikubwa, panga fenicha katikati huku ukiacha hatua kadhaa.

Tenga eneo la mazungumzo

Watu waliokaa sebuleni wanatakiwa kuongea kawaida kwa uhuru bila kupayuka ama kuumiza shingo kumtazama anayeongea naye. Panga sofa na viti kwa mpangilio ambao zitatazama japo si kazima ziwe kwenye mstari ulionyooka bali zikaribiane. Kama sebule ni kubwa sana ni afadhali kuweka maeneo mawili. Wapo watu wenye sebule za hivi ambapo wana kawaida ya eneo moja kukaa wageni na la pili hukaa wenyeji.

Uwiano


Uwiano ni jambo muhimu sana kwenye kupanga fenicha sebuleni. Usipange kubwa tu peke yake na ndogo tu pele yake. Hakikisha unachanganya ukubwa na maumbo tofauti pamoja.

Zingatia pa kupita

Watu wasiruke kochi ili kupita. Kuwe na nafasi ya kutosha angalau hatua moja kati ya meza ya kahawa na sofa na pia viti.



# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2023
SMS - 0713 447766
MWAKA HUU UTOBOI!
JUKWAANI
'TOBO GANI?"
HIVI NDUGU HELA NA UHAI WANGU BORA NINI? MAANA NAKUONA UMEKAZANIA KUNITOA ROHO!
NILIKUSIKIA UKISEMA HILI PAMBANO NIFE AU UFE WEWE! TATIZO LIKO WAPI?
ANDAMANENI KUELEKEA NILIPOSEMA ILA MSIRUDI NYUMA MIE NITAANGALIA KWENYE TIVII
WAHI KWENYE TIVII KABLA WANAO HAWAJAWAHI NAFASI KWENYE MAKOCHI
NIKIWAAMBIA KUWA KUNA MADEREVA WENGI WANAISHI DUNIANI BILA ROHO MTASEMA MANENO YA MLEVI!
USIPOTAJA VITUO MIMI SIO SHIDA ZANGU KILA ABIRIA ANAJUA ANAPOKWENDA
MWENDO WAKO WATU WOTE MAKOO YAME-KAUKA HAYATOI SAUTI!
NIPO CHINI YA MIGUU YAKO NAAPA UKIENDELEA 'KUMSOLOLEA WAIF' NAKUNYONGOLOTA SHINGO YAKO!
ASANTE KWA ONYO LA 'KIDIJITALI'
HII SHUGHULI IMEFANYWA NA WAIF' JANA NIMEJISAHAU BADALA YA KURUDI NA CHIPSI, MIPOMBE IME-NIZIDI NIMERUDI NA 'GOMA!'
HII SHUGHULI AU KAKUGUSAGUSA? MWENZAKO KARUDI NA CHIPSI KAVU HAZINA TOMATO YUPO MONCHWALI
POSTI
MKE WANGU MAKAMO HAYA NICHEPUKE NATAFUTA NINI? NAKOSA NINI KWAKO? KUJICHUNGA KOTE BADO HUNIAMINI TU!
'NASHANGA!
smoll hausi SINZA
...KINYUNYIZO CHA LEO...
"BIA TAMU KAMA UNANUNULIWA"

## HABARI KIMATAIFA

# Charles III atawazwa rasmi mfalme Uingereza

**LONDON,** UINGEREZA

MFALME Charles III jana alitawazwa rasmi kuwa mfalme wa Uingereza katika hafla iliyofanyika katika Kanisa la Anglikana la Westminster Abbey huku ikihudhuriwa na wageni 2,000 wakiwamo viongozi mbalimbali wa dunia na watu maarufu.

Shughuli ya kumtawaza mfalme huyo wa Uingereza ilifanyika wakati utawala wa kifalme nchini humo ukikabiliwa na upinzani.

Ibada ya kumtawaza Mfalme Charles ilisindikizwa na milio ya tarumbeta na shughuli hiyo ilihudhuriwa na wageni mbalimbali wakiwamo, Mke wa Rais wa Marekani, Jill Biden na Rais wa Ufaransa, Emmanuel Macron.

Wengine ni Waziri Mkuu wa Canada, Justin Trudeau, mawaziri wakuu wanane wa zamani wa Uingereza pamoja na Waziri Mkuu wa sasa, Rishi Sunak huku Ujerumani ikiwakilishwa na Rais Frank-Walter Steinmeier.

Askofu Mkuu wa Canterbury, Justin Welby, ndiye aliyemvalisha mfalme huyo taji la dhahabu ikiwa ni ishara ya mamlaka ya utawala wa kifalme katika ibada hiyo ambako Mfalme na mke wake, Camilla, walishiriki pia sakramenti takatifu ya Meza ya Bwana.

Nje ya kanisa la Wesminster Abbey alikotawazwa mfalme huyo kulikuwa na askari wa ulinzi 10,000 pamoja na watazamaji 10,000.

Maelfu ya watu kutoka maeneo mbalimbali ya Uingereza na duniani kote waliweka kambi katika njia yenye kilomita mbili ambayo Mfalme Charles III na mkewe Camilla walipita kwenda Westminster Abbey.

Kundi dogo la waandamanaji walijikusanya kufuata njia iliyotumiwa na mfalme katika safari yake kutoka katika Kasri la Buckingham akiwa kwenye gari lililokokotwa na farasi.

Kwa familia ya kifalme na serikali, tukio la kuvikwa taji kwa Mfalme Charles III ni njia ya kuonyesha urithi na utamaduni duniani kote.

Camilla pia alivishwa taji la umalkia kwenye sherehe hizo. Shughuli hiyo ilitarajiwa kutazamwa na mamilioni ya watu duniani.

**DW**



Charles III (74) ametawazwa kuwa mfalme wa Uingereza, akichukua nafasi ya mama yake Malkia Elizabeth II aliyefariki mwaka jana, katika halfa iliyofanyika kwa mara ya kwanza tangu mwaka wa 1953.**PICHA: MTANDAO.**

# Iran yamnyonga raia wa Uswidi madai ugaidi

**TEHRAN,** IRAN

IRAN imemnyonga mwanamume raia wa Uswidi mwenye asili ya Iran, Habib Chaab anayetuhumiwa kuhusika na shambulio baya la 2018 kwenye gwaride la kijeshi.

Inaelezwa kuwa Chaab alikuwa mwanzilishi wa kundi linalopigania uhuru wa waarabu katika jimbo la Khuzestan kusini magharibi mwa Iran, na kwamba alikuwa akiishi uhamishoni nchini Uswidi kwa muongo mmoja alipotekwa nyara na maofisa wa Iran nchini Uturuki mwaka 2020.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Uswidi Tobias Billstrom, alisema serikali yake imeitaka Iran kutomnyonga Chaab.

"Hukumu ya kifo ni adhabu ya kinyama na isiyofaa na Sweden, mataifa mengine ya Umoja wa Ulaya (EU), yanalaani utekelezaji wake kwa hali zote," alisema.

Mahakama ya Iran ilimshutumu Chaab kwa kuongoza harakati al-Nidal, au Vuguvugu la Mapambano ya ukombozi wa waarabu wa Ahvaz, ambalo Iran inasema ni kundi la kigaidi lililoendesha mashambulizi kusini magharibi mwa nchi hiyo.

Jimbo hilo lenye utajiri mkubwa wa mafuta lina waarabu walio wachache ambao kwa muda mrefu wamekuwa wakilalamikia kutengwa na kubaguliwa, jambo ambalo Tehran inakanusha.

Shambulio la 2018 kwenye gwaride la kijeshi katika mji wa Ahvaz lilishuhudia watu wenye silaha wakiwafyatulia risasi wanajeshi wa Walinzi wa Mapinduzi, na kuua watu 25 wakiwemo wanajeshi na raia waliokuwa wakitazama gwaride hilo.

Chaab aliripotiwa kuhadaiwa na kuletwa hadi Istanbul kukutana na mwanamke kabla ya kutekwa nyara na kusafirishwa hadi Iran katika operesheni inayosemekana kuratibiwa na kiongozi maarufu wa uhalifu wa Iran anayeishi Uturuki.

Hata hivyo, maofisa wa Iran hawajatoa maelezo kuhusu kukamatwa kwa Chaab.

**BBC**

# Mafuriko yasababisha vifo182 DRC

**KINSHASA,** DRC

WATU 182 wamefariki kutokana na mafuriko na maporomoko makubwa ya ardhi katika eneo la mashariki ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) huku mamlaka za eneo husika zikisema kuwa idadi hiyo inazidi kuongezeka.

Mamlaka za ndani zilisema jana kuwa, wafanyakazi wa misaada ya kibinadamu nchini DRC, wamepata miili hiyo katika kijiji cha Bushushu, na kwamba wengi wao ni wanawake na watoto.

Gavana katika eneo hilo Theo Ngwabidje, alithibitisha vifo vya watu hao kwa shirika la Habari la Ujerumani (DPA) na kusema kuwa huenda vifo zaidi vikaripotiwa.

Vile vile, Rais wa DRC Felix Tshisekedi, ametangaza rasmi kuwa siku ya jumatatu itakua siku maalum ili kuomboleza kama taifa.

Msemaji wa serikali, Patrick Muyaya, alieleza kuwa baadhi ya mawaziri watakwenda kwenye eneo la tukio kwa ajili ya kupanga shughuli ya utoaji misaada na jinsi ya kusimamia shughuli za kupambana na majanga kama hayo.

Hata hivyo, ilibainishwa kwamba katika maeneo mbalimbali nchini humo mvua kubwa hushuhudiwa hadi mwisho wa mwezi mei.

Aidha, wakati hayo yakiendelea DRC, nchi jirani ya Rwanda pia iliomboleza vifo vya watu zaidi ya 130, waliofariki kutokana na mafuriko yaliyokumba eneo la magharibi mwa nchi hiyo, huku mamia ya nyumba ziliharibiwa.

Ilielezwa kuwa maombolezo hayo yatafanyika wakati serikali ikiendelea kukadiria hasara iliyotokana na mafuriko hayo, huku shughuli za mazishi pia zikiendelea katika moja ya majanga mabaya zaidi kuwahi kuikumba nchi himo.

Pia inaelezwa kuwa wengine mbali na kupoteza ndugu zao, walisema shughuli za maisha ya kawaida zimekoma rasmi baada ya kupoteza mali nyingi ambazo walikuwa wakizitegemea kukimu familia zao.

**RFI**


## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

Ndugu **ANDREA JAMES MTABAZI** anatangaza kupotelewa na kadi yake ya Pikipiki aina ya **HAOJUE** yenye namba za usajili MC 410 CTV.

Ametoa taarifa polisi na kupewa namba **MOR/MOR/RB/152094/2023**

Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi kilicho karibu naye.



**JAMHURI YA MUUNGANO W A TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA MOROGORO**
**SHAURI LA MAOMBI MADOGO YA MADAI NA. 22 YA 2022**

**ANTHONY CHIKOTI.......................MWOMBAJI**
**DHIDI YA**
**WILLIUM BEATUS LIMBE .................. MJIBU MAOMBI**

**WITO WA MAHAKAMANI**

**KWA: WILLIUM BEATUS LIMBE**

Wito huu ni wa kesi tajwa hapo juu, ambayo imepangwa kutajwa tarehe 29 mwezi wa 5 mwaka 2023 saa 03:00 asubuhi mbele ya Mheshimiwa **Jaji M.J. CHABA.**

Unatakiwa kuhudhuria wewe binafsi au wakili uliyemuidhinisha kusimama kwa niaba yako na pia unatakwia kutoa maelezo yako siku hiyo na nakala zote za ushahidi utakazo tumia kwa shauri hili .

Zingatia kwamba , kutohudhuria siku ya kesi na kwa wakati uliotajwa hapo juu, Mahakama itaendelea kusikiliza shauri hili na kutoa maamuzi bila ya uwepo wako.

Imetolewa chini ya Muhuri wa Mahakama Kuu Kanda ya Morogoro leo siku ya tarehe **2 mwezi wa 05 Mwaka 2023 .**

NAIBU MSAJILI MAHAKAMA KUU
MOROGORO



## KUPOTELEWA NA CHETI



**KHAMIS ABDALLAH SHAA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index number S1838/0051 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia MBARALI PREPARATORY SEKONDARI mwaka 2016. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/CEN/RB/156146/2023.**

MAKALA

# VYOMBO VYA HABARI NI CHACHU



Na Magabilo Masambu

KILA ifikapo Mei 3, kila mwaka, dunia kwa ujumla huadhimisha Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari. Kwa mujibu wa Umoja wa Mataifa (UN), maadhimisho ya mwaka huu ni ya 30 ambayo yameandaliwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) yaliyofanyika kwenye makao makuu ya umoja huo, New York, Marekani.

Nchini Tanzania, mwaka huu maadhimisho hayo yalifanyika Zanzibar. Wanahabari na wadau wa vyombo vya habari walipata nafasi ya kushiriki mjadala juu ya uhuru wa habari nchini.

Safari ya uhuru wa vyombo vya habari imekuwa ya miongo kadhaa toka zamani.

Kama tunavyofahamu, vyombo vya habari vinatumika zaidi kuwafanya wasioonekana waonekane, lakini bahati mbaya ni kwamba wakishaonekana wakapata bahati ya kushika nafasi za madaraka, wengi wao hugeuka na kuwa maadui wa vyombo vya habari kwa kulinda maslahi binafsi.

Nchi nyingi duniani zimegoma kuufanya muhimili wa habari kuwa muhimili kamili kisheria kama ilivyo Serikali, Bunge na Mahakama.

Hii yote ni kutaka vyombo vya habari na tasinia kwa ujumla kuendelea kutazamwa pale inapoandika habari zinazowahusu watawala, hasa kuhusu madhambi yao kwa wananchi na serikali wanazoziongoza.

Wako wanaotafsiri kwamba kuwapo kwa wingi wa vyombo vya habari ni alama kamili kuonyesha kwamba, sasa uhuru wa kuhabarisha umma ni mkubwa. Jambo hili linafanana na wingi wa vyama vya siasa, unavyotafsiriwa kama dalili ya kuonyesha ukuaji wa demokrasia.

Uhuru wa vyombo vya habari haupimwi kwa kuwa na vyombo vingi vya habari, bali aina za habari zinazotolewa na vyombo hivyo.

Ni kweli kwamba nchi ikiwa na chombo kimoja cha Habari, uhuru unakuwa umeminywa zaidi. Vilevile vikiwa vingi basi viwe na uwezo wa kuripoti habari ambazo viongozi wasingependa kuzisikia, lakini wananchi wakazisikia kwa maslahi ya nchi.

Hii ni kwa sababu wananchi ndio wanaowaweka viongozi madarakani kwa mujibu wa Katiba.

Kwa lugha nyepesi ndio waajiri wa viongozi hao, hivyo ni muhimu kuyafahamu mazuri na mabaya ya viongozi wao ili inapofika vipindi vya uchaguzi wawe na uwezo wa kuchambua ipi ngano na ipi ni pumba.

Upande wa pili, serikali ikiruhusu uhuru wa habari na kujieleza kwa watu kitendo hicho kitarahisisha serikali kufahamu wapi upungufu uliko ili kuyafanyia kazi na kuleta imani kubwa kwa wapigakura.

Kwa hiyo, vyombo vya habari na serikali kwa ujumla ni nyenzo muhimu katika ustawi wa maisha ya watu, ikiwa kila mmoja atatambua jukumu lake kwa nyakati tofauti.

Tulishuhudia mambo yalivyokuwa huko nyuma, leo tunayaona mabadiliko kwa sababu aliyebadilishwa ni mtu. Kesho hatuna uhakika kama atakayekuja atalinda angalau hata kwa kiasi kidogo cha uhuru huo.

Sheria zetu za vyombo vya habari zimesalia zile zile, kwa hiyo atakayekuja ana uwezo wa kuchagua azitumie au aziache kando kwa muda.

Uhuru wa vyombo vya vyetu vya habari unakuwa kama ule mchezo wa kumfumbata nzi mkononi ukiwa umekuja ngumi akiwa hai, kisha unamuuliza rafiki yako kwamba "nzi huyu amekufa au yuko hai?" Akisema yuko hai unamminya anakufa, akisema amekufa wewe unamwachilia anaruka.

Sasa hatutaki hako kamchezo tunataka kuona wazi, kama nzi amekufa au yuko hai kwa kurekebisha sheria za vyombo vya habari ili yeyote atakayetokea asiwe na uwezo wa kuamua uwapo huru au la.

Pamoja na yote, waungwana wanasema, mnyonge mnyongeni haki yake mpeni.

Hii ni kusema kuwa Rais Samia Suluhu Hassan pamoja na kuwapo sheria kandamizi za uhuru wa vyombo vya Habari, hasa Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari ya Mwaka 2016 na Sheria ya Magazeti ya Mwaka 1976, bado uhuru wa watu kujieleza katika awamu hii na hatujasikia matukio ya watu kutekwa na kupotea kama ilivyokuwa nyakati fulani.

Ni muhimu kwa nchi kufahamu kuwa uhuru wa vyombo vya habari ni nyenzo muhimu sana katika maendeleo ya mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

Vyombo vya habari vimekuwa vikiibua matatizo mbalimbali katika jamii, ambayo mengine yanapata ufumbuzi wa moja kwa moja.

Vinaibua ufisadi wa baadhi ya viongozi kazi inasalia kwa vyombo husika kuchukua hatua, hivyo kwa namna yoyote ile, uhuru wa vyombo vya habari ni muhimu katika maendeleo, kama vitatumika na kutumiwa vizuri.

Kwa wanahabari, jambo la msingi ni kuwa wazalendo kwa nchi kwa sababu kalamu inasadikika kuwa silaha mbaya zaidi kuliko bunduki.

Kwa hiyo ni muhimu kuitumia vizuri kwa manufaa ya nchi na watu wake.

Ni kweli kwamba vyombo vyetu vinajiendesha kibiashara, bila habari za kuuza itakuwa ngumu kusomwa ama kutazamwa, lakini hili lisifanye tusiandike na kuripoti habari zinazowahusu wananchi wa kawaida, eti kwa sababu habari hizo haziwezi kuuza.

**0688157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**DAR ES SALAAM-TANZANIA**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# *Kosa mama kunizaa mtoto mwema, kupenda watu duniani nadhulumiwa*



Na Adam Fungamwango

MAPENZI ni ugonjwa mbaya sana kuliko wowote ule duniani. Hata kama unaumwa magonjwa ya kawaida, kama ukijua kuna mtu anakupenda unafarijika. Duniani hata kama ukiwa na pesa nyingi, ukijua kuwa watu wanakupenda kwa ajili ya pesa zako na si mapenzi ya kweli, unaweza kuchanganyikiwa na hutojisikia vizuri.

Mapenzi ni kitu cha ajabu sana. Mtu akipenda au kupendwa anatamani hata aote mbawa na kuruka juu kuutangazia ulimwengu jinsi anavyopenda au kupendwa.

Hebu fikiria, una mpenzi ambaye umependana naye sana, lakini mwisho wa siku kuna watu wanamrubuni na kumchukua. Ni lazima utahangaika kutaka kulirudisha penzi kwa nguvu zote. Ukishindwa inakuwa ni huzuni, na mateso.

Hapa kuna mtu amedhulumiwa penzi. Amelalamika kweli. Ameongea kwa hisia kali sana inayoweza kumtoa machozi mtu yeyote yule.

Mtu huyu yumo kwenye wimbo wa Maya, ambao umeimbwa na mwanamuziki Mafumu Bilal (marehemu).

Hata hivyo, asili ya wimbo huu 'Maya' ni TP OK Jazz ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo chini ya Franco Luambo Luanzo Makiadi.

Ni wimbo uliofyatuliwa mwanzoni mwa miaka ya 1980 ukitungwa na Lutumba Simaro Masiya, mmoja wa viongozi wa bendi hiyo na mpiga rhythm, ambaye alifariki dunia mwaka 2019 akiwa na miaka 81. Wimbo huo uliimbwa kwa lugha ya Kilingala na Lassa Ndombasi ambaye mashabiki wa muziki wanamfahamu kwa jina la Carlito Lassa.

Kama kawaida ya Mzee Lutumba, tungo za nyimbo zake zimejaa hisia kali sana na mara nyingi huwaliza wengi, na wengine hujiuliza huwa anawaza nini, au hukaa wapi anapotunga hadi anapata aina ya maneno anayoyatumia.

Mzee Simaro alitunga wimbo unamhusu mtu mmoja aliyenyanyasika kimapenzi.

Alichofanya Mafumu ni kuutafsiri kwa kiswahili lakini akatumia kiswahili ambacho Watanzania wengi walisema ni kibovu, ila alichotumia ni cha Kikongomani tena kile cha Lumbumbashi. Hapa nimejaribu kukiinyoosha ili wasomaji waelewa nini kimeimbwa. Kama ulishawahi kusikia nyimbo za wanamuziki na wasanii wakilalamika kuachwa, kukimbiwa au kunyanyaswa kimapenzi, huu ni kiboko.

Si zile za mpenzi wangu umeniacha mimi nateseka, sili silali juu yako, rudi mpenzi nakukumbuka, hapana. Hapa mwanaume analalamika kweli kweli. tupitia mashairi ya wimbo huo ' Maya' kama yalivyowekwa kwa lugha ya kiswahili, kutokana na wimbi kama huo wa TP OK Jazz.

"Maya nakamata maneno kichwani maneno yananipita rohoni, naanza kuhesabu masiku kwa vidole, tabu inanikamata, mara ya kwanza tulifanyaga matata, hatukupatana iye, kama nisingefungua macho, ulitaka kunikataa ee.

Maya naweka mkono kwenye shavu, maneno yananipita rohoni, naanza kuchapa kalamu kwa udongo, kizunguzungu kinapita, wakati ulipita ulisemaga tuachane, nikataa iye, kama nilingependa treni kukufuata, hukutaka kurudia.

Maya najiumiza meno kuulimi damu inachanga na mate mukinywa, nyingine nameza nyingine natema, kizunguzungu kinapita, wakati ulipiga ulisemaga tuachane, nikakataa iye, kama nigefuatage upuuzi wako, ilikuwa ndiyo tuachane."

Jamaa anaanza kumlalamikia mpenzi wake tabu aliyoipata siku za nyuma akijaribu kuzuia jaribio la kutorokwa.

"Ooh mama nalia akili mu kichwa, maneno naona sisadiki, nakuwa kama mtu alikwisha, kizunguzungu pa macho, mtu alikuwa mtumishi wetu, leo anakuwa bwana, nifanyeje Maya nakuwa kama mgonjwa wa wazimu ee.

Hata iwe vipi, mtu hawezi kusahau mlango wetu, hasa mimi nasema hatukusikizana hivyo. Tabu na raha yote ni nyumbani kwetu, ugomvi na wivu kwenye macho ya watu, nazoea kukubembeleza.

Hata iwe vipi, njoo nikubembele, lakini kwa kunikataa, hatukusikilizana hivyo." Mwanamke anabembelewa hapo.

"Mungu aliumba neno mapendo aliumba mateso, leo nilikuwa nalilia munyumba, Mungu ananitumia muzimu ee. Mie nakuwa na ukubwa mbaya, mikosi duniani, haina neno Maya olewa lyako, nafunga mikono yangu.

Mtu alikuwa ananipikiaga sombe, leo inakuwa nyoka, majivuno nilikuwa najivuna inakwenda yote na maji.

Hapa munaninyang'anya Maya atagomboa nani, naenda kulia kati ya mvua nakatala, machozi yabakie alama kumuso. (Hataki kwenda kulia kwenye mvua, ili machozi yabakie alama usoni).

Hii kosa ya mama, alizaa na wema, wema wa kupenda watu mu dunia, wacha nidhulimiwe eee."

Maya anaondoka kwenda kuolewa, jamaa analalamika majivuno yote sasa kwisha, anasema hii yote ni kosa la mama yake amemzaa na wema, anapenda watu duniani, lakini wanamdhulumu Maya wake.

Ananyang'wanywa Maya, atamgomboa nani? Atampata wapi? Atamnunua wapi tena?

"Maya kama siku nyingine utaona ndoto usiku jua mimi ni wako niko nakulilia, shida sikitiko na mawazo, kwani tumezoeana, mwisho dunia nini? mapendo yetu yachache?

Maya kama iko namna, umlilie mume mwenzangu ee, siku utabeba mimba umuombe ruhusa, mtoto wa kwanza utazaa awe mtoto mwanaume awe mzuri kama wewe, umpe jina la Marlone, mwisho wa dunia nini mapendo yetu yachache?

Mungu aliumba aliumba neno mateso, aliumba mateso."

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

# Simu ya Sumu-9

MIEZI miwili tu baada ya ndoa, Husna anapigiwa simu ya mtu asiyemfahamu. Haikuwa simu ya heri. Ni simu ya mtu anayeonekana amedhamiria. Amedhamiria kufanya kitu alichokikusudia. Kwenye maisha ya ndoa aliambiwa yatakuwa ya shida na raha, lakini kwake haikuwa mapema kiasi hicho. Alihisi sasa hakuingia kwenye ndoa aliyoikusudia bali ni ndoa ndoana.Ni nani aliyempigia simu Husna? Alitaka nini? Lengo lake hasa ni nini? Ni kweli alichokusudia mpiga simu ndicho alichokihitaji ili kuvuruga ndoa hiyo? Nenda hatua moja moja kwa kusoma kila nakala ya toleo la Nipashe ili upate ukweli mzima wa kisa hiki cha utata, kusisimua, kusikitisha na chenye mafunzo makubwa kwa jamii na wanandoa wote.

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

WIKI ijayo siku ya Jumapili nina kijipati nyumbani. Yule mwanao Tima, anatimiza miaka mitano sasa tangu kuzaliwa, kwa hiyo nimeandaa kisherehe kidogo cha 'bethdei' yake. Kwa hiyo nakuomba usikose nyumbani."

Kwa akili yake Dan hakutegemea hilo. Alidhani huenda kaka yake alikuwa na kitu kikubwa kuliko hicho. Kitendo cha kufunga safari na kwenda nyumbani kumwalika rasmi kama mtu baki, kilimshangaza kidogo.

"Sasa kama ni hivyo si ungeniambia tu kwenye simu, yaani umeacha shughuli zako na mvua hii nilidhani jambo ni kubwa sana!"

"Nina maana yangu Dan. Ningekupigia simu na wewe ungechukulia kisimusimu tu. Siku hiyo unaweza kupata kijidharura kidogo, ukanipigia simu ukaniambia siji. Lakini hii nimeamua kuja mwenyewe kwa sababu nataka uwapo nyumbani siku hiyo, ni muhimu sana, usikose."

"Sawa kaka mimi nitakuja, wala haina shida."

"Enhe, umepata mwanamke mwingine au?" Lilikuwa kama swali la mtego hivi.

Dan akacheka halafu akajibu "Nina hamu na mwanamke kaka? Hili lenyewe limenishinda."

"Sasa si umlete basi yule aliyempigia simu Husna, maana kaharibu halafu hataki kuja kuchukua nafasi."

Maneno hayo yalimfanya kucheka tena. Lakini safari hii ilikuwa ya maumivu ndani yake. Akakumbuka alichopitia wiki moja iliyopita.

"We kaka we, yaliyonikuta ni siri yangu mwenyewe. Lakini kwa sababu umenichokoza, ngoja nikwambie. Si nilikwambia nitaenda kwa Ziada. Nilichokipata huko Mungu mwenyewe ndiye anajua.

Aliniruka futi mia kwenda juu, akakataa katakata, halafu akanipakia maneno ya ajabu, we acha tu. Na kaniambia tayari yeye ana mchumba anataka kuolewa kwa hivyo hawezi kufanya hivyo. Nikatoka hapo, nikaenda kwa mke wangu, bwana wee, yeye na mama yake hawakuniacha bure, walinipakia maneno hayo, nikatoka mbio."

*********

"He! Shemeji yangu leo kuna nini, maana si kawaida yako." Ilikuwa sauti ya Husna akimkaribisha Belo nyumbani kwake.

Hakutarajia hilo. Alikumbuka siku ambayo alikuja nyumbani kwao na maneno makali aliyoongea, hakudhani kama atapokelewa kirahisi namna hiyo.




**Mtu yule alikuwa akipiga hatua moja baada ya nyingine kuelekea anakoelekea. Mtu mwingine alikuwa nyumbani kwake. Alikuwa amepigiwa simu kuwa atafika nyumbani jioni siku hiyo. Na kwa sababu siku hiyo hakuwa na kazi nyingi na mizunguko pia, alirejea nyumbani mapema kumsubiri mgeni wake.**

"Labda hasira zimemuisha." Alijisemea moyoni. Akakumbuka jinsi alivyokuwa akilalamika.

"Hivi kumbe nyinyi mnajua kama kaka yenu ana mwanamke mwingine?

Shemeji Belo? Wifi zangu, hivi kumbe ninyi ndugu mnajua kama kaka yenu ana mwanamke mwingine halafu hamniambii? Wote ninyi mnakuja kwangu nawakaribisha kwa furaha, nawapikia chakula, tunacheka na kufurahi kumbe mnaning'ong'a kisogo? Mmenifanya mimi kama taahira. Nimewakosea nini mimi?"

Kumbe nyinyi ndugu kuna vitu vimo ndani ya mioyo yenu? Mmenifanya mimi kama taahira. Sasa kwa nini kaka yenu alikuja kunioa mimi? Alikuja kunioa ili anidhalilishe?

Ndoa ina miezi miwili tu, imeanza matatizo hivi? Tutafika kweli? Hili mlikuwa mnalijua, haiwezekani ndoa bado changa hivi halafu kuna mtu anajitokeza kutaka kuivunja ndoa yangu. Ina maana huyo mtu alikuwa naye muda mrefu kabla ya mimi? Sasa kwa nini kaja kunioa mimi kama si kunidhalilisha? Kwa nini hakumuoa huyo? Kwa nini wanaamua kunivunjia nyumba yangu mapema hivi? Kwa nini wameamua hivi? Mimi hata siamini. Sasa kwa nini mnaniita wifi na shemeji, wakati mna shemeji wifi wengine?"

Ni maneno ambayo yalirudia tena kichwani mwake kama yaliyorekodiwa na redio kaseti au televisheni na kurudia tena. Aliliona kama tukio lile limetokea jana tu. Na kila anapomtazama usoni yanajirudia tena na kushindwa kumtazama sawa sawa shemeji yake kwa aibu.

Kabla ya kwenda kwake alikuwa amejipanga kimkakati, maneno mengi ya hekima na busara pamoja na samahani kibao, lakini kwa jinsi alivyopokea, ilimshangaza.

"Pita karibu ndani shemeji yangu." Husna akamkaribisha.

"Hapana shemeji, mimi nadhani tungekaa huku huku nje, au twende sehemu karibu hapo kwenye kioski, tunwe soda huku tukiongea kidogo." Aliomba Belo.

"Hapana, haiwezekani shemeji yangu nikupeleke sehemu nyingine zaidi ya hapa nyumbani kwetu. Hakuna tatizo tuingie ndani, wewe ni shemeji yangu tu." Akaongea kwa sauti ya bashasha na tabasamu juu iliyomuondoa hofu Belo.

Akaongozwa ndani na kusalimiana na mama yake mdogo Tabia. Akakaribishwa kwenye kochi. Baada ya kusalamu na matani ya hapa na pale. Kila mmoja alikuwa na shauku ya kutaka kujua nini hasa kitaendelea.

Husna alikuwa na hamu ya kutaka kujua kilichomleta shemeji yake pale wakati haikuwa kawaida yake. Belo alikuwa na hamu ya kutaka kujua nini kitaendelea atakapokimwaga kile kilichompekeleka. Ukimya dakika mmoja ulitawala.

Belo alivuta pumzi ndefu na kuishusha. Ikampa nguvu ya kuanza mazungumzo.

"Shemeji huu mguu unaouona ni wako." Alianzisha mazungumzo na Husna alikaa kimya bila kujibu chochote akiendelea kumsikiliza kwa makini.

"Nimekuja hapa kwa lengo la kukukaribisha kwenye kijisherehe nyumbani kwangu." Ni maneno ambayo yalimshusha presha Husna, lakini ilikuwa karibu aangue kicheko.

"Shemeji bwana, yaani umetoka nyumbani kote huko kuja kunialika, halafu kitu chenyewe unasema kijisherehe kweli?" Akamwuliza, halafu sasa kile kicheko alichota kucheka mwanzo akakiachia. Belo naye ilibidi amuunge mkono, halafu akasema.

"Usicheke shemeji, sasa ukisema sherehe hapa, unaweza kudhani ya harusi, mimi naona, au sherehe kubwa, kwanza hii siyo sherehe nimekosema kiswahili ni pati tu, au naweza kusema kijipati."

"Mhh! Shemeji, haya, hicho kijipati kinasemaje na cha nini?"

"Ni cha 'bethdei' tu, binti yangu Tima anatimiza miaka mitano. Nimealika watu kadhaa, pamoja na kwamba kwa sasa umetengana na mdogo wangu, bado mna mtafaruku bado hamjapeana talaka, mimi nimekuja kukualika kama shemeji yangu, ukusanyike pale na wanandugu wengine kwa ajili ya pati. Na hata wifi zako wamenituma hilo."

"Kwanza mimi nashukuru kuona kumbe bado mnanikumbuka shemeji yenu. Mimi nilidhani umekuja kwa ajili ya suala la kutupatanisha na ndugu yako. Hilo kwa sasa sahau kabisa shemeji. Pia mimi sina tatizo kwa sababu mpaka kutoka huko kuja huku ina maana mnanithamini sana, lakini mimi ninachoogopa ni ugomvi!"

"Ugomvi gani tena huo shemeji?" Akashangaa Belo.

"Huyo kidudu mtu aliyenipigia simu kunitukana. Si alisema nyinyi mnamfahamu. Inawezekana wewe shemeji humfahamu, lakini dada zake wakawa wanamfahamu. Anaweza kuja baada ya kutukanana kwenye simu, sasa zikalika ngumi nyumbani kwako.

Halafu shemeji, hata Dan si atakuwepo, kutakuwa na usalama kweli, mimi na Dan hatuelewani. Halafu kwa bahati mbaya ndiyo akaja na huyo hawara yake itakuwaje?"

**ITAENDELEA JUMAPILI**




# Jina la mtoto wa Kardashian hadharani

Hatimaye wanandoa Khloe Kardashian na Tristan Thompson wameweka wazi jina la mtoto wao wa kiume lililokuwa likisubiriwa na watu wengi.

Mtoto huyo wa kiume ametajwa kuwa ni Tatum Robert. Kwa mujibu ya majarida ya nchini Marekani, na wanandoa hao ni kwamba walikuwa na chaguo lingine la Robert Tatum.

"Kulikuwa na mazungumzo juu ya kama anapaswa kuwa Tatum Robert au awe Robert Tatum," chanzo kilisema katika nakala iliyochapishwa Alhamisi.

Mtu wa ndani alisema familia ilikuwa inaegemea zaidi kwenye jina la Robert kwa sababu ya kumheshimu baba yake, Rob Kardashian.

"Baadhi ya familia walikuwa wakiegemea zaidi kwa Robert, kwa sababu inamheshimu baba yake Kardashian, Robert, aliyefariki mwaka mnamo 2003 kwa saratani.

Ikaelezwa kuwa Khloe alitaka jina ambalo halikuwa la kawaida, lakini siyo nje sana na linaloambatana na jina T, na ndipo likaja jina la Tatum, kilieleza chanzo hicho.



# IZZO BIZNESS AJA NA 'FINE' YAKE

Mkali ya bongo fleva, Izzo Bizness ameibuka ghafla na ngoma kali aliyoita Fine akishirikisha Lody Music.

Ngoma hiyo aliiweka juzi kwenye mtandao wa 'YouTube' na kwa muda mfupi imeanza kubamba na kukubaliwa kwa mashabiki wake na wamuziki wa bongo fleva kwa ujumla.

Hata hivyo, Izzo ameitoa ngoma hiyo kwa mfumo wa audio' na mashabiki wake wanasubiri kwa hamu pale atakapoitia kwa mfumo wa video.

Msanii hiyo ameshatoa ngoma mbalimbali kwa miaka mingi ambazo zimekuwa zikifanya vizuri kwenye tasnia ya muziki huo.

Ngoma hizo ni kama 'Umeniweza', 'Kidawa', 'Rafiki', 'Nishadata', 'Tumeoana' na nyingine nyingi huku akiwashirikisha wasanii mbalimbalia kama Mwana FA ambaye kwa sasa ni Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, jina lake halisi akiwa na Hamisi Mwinjuma, pia ni mBunge wa Muheza, kwenye ngoma ya 'Shame Lake', Jay Melody, Barnaba, Juma Nature na wengine wengi.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### DAU LA RICE LATAJWA

WEST Ham itahitaji kulipwa pauni milioni 100 ili kumwachia kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya England, Declan Rice mwenye umri wa miaka 24 katika msimu huu wa joto. (***ESPN***)

### MARTINEZ ANUKIA LIVERPOOL

CHELSEA inapania kumnunua mshambuliaji wa Inter Milan, Lautaro Martinez, msimu huu wa joto. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina mwenye umri wa miaka 25 pia analengwa na Manchester United. (***Football Insider***)

### ONANA SAFI CHELSEA

CHELSEA inataka kumfanya mlinda mlango wa Inter Milan na Cameroon, Andre Onana, mwenye umri wa miaka 27 namba moja msimu ujao na wana uhakika wa kumsajili Mauricio Pochettino kama kocha wao mpya. (***Telegraph***)

### BELLINGHAM BEI JUU

KIUNGO wa kati wa Borussia Dortmund na England, Jude Bellingham (19), atatia saini mkataba wa miaka sita na Real Madrid msimu huu, ambao utamfanya kuwa mchezaji wa pili anayelipwa fedha nyingi kwa miamba hao wa Hispania baada ya mshambuliaji wa Ubelgiji, Eden Hazard (32). (***SER Deportivos, via Mail***)

### FRIMPONG KUTUA UNITED

KOCHA wa Manchester United, Erik ten Hag, anataka kumsajili beki Mholanzi Jeremie Frimpong mwenye umri wa miaka 22 kutoka Bayer Leverkusen msimu huu. (***Mirror***)

### WEGHORST NJIA MOJA

KLABU ya Manchester United haina mpango wa kumsajili Wout Weghorst kwa mkataba wa kudumu. Mshambuliaji huyo wa Uholanzi mwenye umri wa miaka 30 alijiunga na United kwa mkopo kutoka Burnley. (***Manchester Evening News***)

### MODRIC AULA MADRID

KIUNGO wa kati wa Timu ya Taifa ya Croatia, Luka Modric mwenye umri wa miaka 37 anatazamiwa kuongeza mkataba wake Real Madrid hadi 2024. (***Relevo***)

### CITY KUMSAJILI BRITS

KLABU ya Manchester City inakaribia kukamilisha dili la kumsajili kipa wa timu ya taifa ya England ya chini ya miaka 16, Spike Brits kutoka AFC Wimbledon. (***Fabrizio Romano***)

### SUTALO ANUKIA ARSENAL

ARSENAL inawanyatia mchezaji Dinamo Zagreb mwenye umri wa miaka 23 na beki wa Timu ya Taifa ya Croatia, Josip Sutalo. (***Evening Standard***)

### WEST HAM KUTIKISWA

KLABU ya West Ham ina wasiwasi kuhusu kumpoteza kiungo wa kati wa Jamhuri ya Czech, Tomas Soucek mwenye umri wa miaka 28, msimu huu wa joto, pamoja na nahodha wao na kiungo wa kati wa England, Declan Rice (24). (***Football Insider***)

### NELSON AGEUKA LULU

REISS Nelson amekataa pendekezo la kwanza la mkataba mpya lililotolewa na Arsenal, huku klabu nyingi nchini England na pia nje ya nchi zikitaka uhamisho wa bure kwa winga huyo wa England mwenye umri wa miaka 23. (***Fabrizio Romano***)

## DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# LAMPARD ATOBOA SIRI INAYOIMALIZA CHELSEA

### Asema wachezaji wapya bado hawajapata muunganiko mzuri na kupelekea kukosa...

**LONDON,** England

WACHEZAJI wapya wa Chelsea hawajapewa fursa ya kupata muunganiko unaohitajika kujenga timu itakayoshinda, hiyo ni kwa mujibu wa kocha wa muda wa kikosi hicho, Frank Lampard.

**The Blues hao walioneka na kutokuwa na mpango wowote wa ushindi wakti walipochezea kichapo cha mabao 3-1 kutoka kwa Ar senal Jumanne iliyopita , kikiwa ni kipigo cha sita mfululizo ambacho kime wafanya kuzama hadi na fasi ya 12 katika msiamo wa Ligi Kuu England.**

Wachezaji kadhaa waliosajiliwa katika dirisha la Januari wameshindwa kufanya vyema, huku Mykhailo Mudryk na Noni Madueke walionunuliwa kwa fedha nyingi wakishindwa kudhihirisha vipaji vyao.

Madueke angalau alifunga bao lake la kwanza kwa klabu katika kupoteza huko pale Emirates, jambo ambalo Mudryk, ambaye aligharimu pauni milioni 88 licha ya kucheza mechi 44 za kikosi cha kwanza akiwa na Shakhtar Donetsk, bado hajafanikiwa.

Kumekuwa na uthabiti mdogo katika kikosi cha kwanza, jambo ambalo lilionekana wazi chini ya bosi wa zamani, Graham Potter na limeendelea katika kipindi kigumu cha mpito cha Lampard.

Chelsea imeunda kikosi kisicho na usawa, kilichojaa vipaji vya ubunifu lakini bila mtu wa kufunga mabao, kuonekana kutounganishwa zaidi uwanjani.

"Namba zinaonyesha sisi ndio timu inayobadilisha zaidi kikosi cha kwanza kuliko timu yoyote," alisema Lampard.

"Kuingia kwa wakati huu kwangu, ni kujaribu kutafuta muunganiko na ushirikiano katika timu ambayo ni muhimu kama sisi sote tunajua.

"Timu kubwa ambazo tumeshuhudia kwa miaka mingi, unaweza kutaja muunganiko kila wakati.

"Unapojaribu kupata hiyo, ni ngumu, na nadhani ni muhimu kujua kwamba tunapokuwa katika hali mbaya na mambo hayo hayajatatuliwa, ni ngumu sana kupata uthabiti wa kile unachotaka.

"Unaishia kuitafuta, na labda ndio sababu watu wanaiita mpito. Hiyo ni changamoto. Kwa msimamo wangu kadiri tunavyotaka matokeo, tunahitaji pia kujaribu kupata muunganiko wa timu kwenda mbele.

"Baadhi ya wachezaji wachanga ambao wameingia kwenye klabu labda hawajapata nafasi ya kutulia, kujisikia vizuri ndani ya timu, kuelewa mabeki wa pembeni watapishana nao, au wachezaji wa kiungo wanaowaunga mkono.

"Huo ni mchakato, na unahitaji kazi. Labda ni kazi ambayo sijaweza kufanya katika jukumu hili kama la muda."

SportPesa | LIVE IN PLA

MECHI KALI
AZAM
VERSUS
SIMBA
1 | 4.85
X | 3.12
2 | 1.55

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# TULIA MARATHON 2023 YAFUNIKA, SIMBU ASIFU



**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

KWA mara nyingine mbio za Mbeya Tulia Marathoni (MTM) zilizofanyika jijini hapa zimetikisa jiji huku wanariadha, Alphonce Simbu na Gabriael Geay wakiendelea kuteka mashabiki wa mchezo huo kwa kushangiliwa wakati wote walipokuwa wanakimbia.

Mbio hizo zilizodhaminiwa pia na Kampuni ya michezo ya kubashiri matokeo ya Betika ziliongozwa na Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Tulia Ackson.

Akizungumza jana kwenye Uwanja wa Sokoine, Dk. Tulia alisema mbio hizo zimelenga kukusanya fedha kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya afya na elimu.

Tulia aliwashukuru washiriki na wadhamini wote kwa kusapoti na kuzidi kuwavutia wakimbiaji kutoka maeneo mbalimbali ndani na nje ya Tanzania.


"Kila mshiriki aliyepo hapa amehusika katika kuboresha miundombinu ya afya na elimu," alisema Dk. Tulia wakati akiwakabidhi zawadi kwa washindi.

Simbu alisema mbio hizo zimejitofautisha na nyingine kwa kutoa fursa kwa wakimbiaji wa mbio za uwanjani na barabarani kukimbia na kupata zawadi.

"Imeongeza hamasa kubwa kwa wanariadha wa mbio zote, fupi, za kati na mbio ndefu," alisema mwanariadha huyo maarufu.

Betika pia iliwadhamini wakimbiaji 60 ambao walishiriki mashindano ya Ligi ya Sodo kukimbia kwenye Mbeya Tulia Marathon msimu huu ikiwa ni moja ya sapoti yao katika kuunga mkono juhudi za serikali kuendeleza michezo hapa nchini.

# Phillips njia panda City



**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola amesema majaliwa ya Kalvin Phillips ndani ya kikosi cha Manchester City yapo mikononi mwake mwenyewe.

Mchezaji huyo aliyesajiliwa kwa pauni milioni 42 majira ya joto ameichezea City mechi nane pekee za Ligi Kuu England, zote akitokea benchi.

Phillips alikabiliwa na tatizo la mapema pale City baada ya kufanyiwa upasuaji wa bega Septemba, mwaka jana lakini tangu aliporejea Novemba ameshindwa kumtoa Rodri kwenye safu ya kiungo ya Guardiola, huku John Stones pia akitoka nje ya ulinzi na kucheza katika nafasi ya juu zaidi.

"Inategemea mchezaji wenyewe," alisema Guardiola.

"Mwisho tuko hapa, ninajaribu kuwa mkweli kwa maswali na hisia zangu.

"Hisia zangu nyakati fulani hubadilika. Lakini mwisho wachezaji ni mali ya klabu, wanatakiwa kujiridhisha wenyewe na timu na si kwa sababu nasema kitu."

HABARI MICHEZO

CHEZA USHINDE KASINO

# TARIMO, KABWEBWE WASHINDA SUPA JACKPOT BONUS WIKI HII

**Na Mwandishi Wetu**




KAMPUNI ya Kubashiri na burudani SportPesa, imeendeleza jadi yake ya kuwawezesha Watanzania kupitia bidhaa yake ya Jackpot ya katikati ya wiki na Jackpot ya mwisho wa wiki yaani Supa Jackpot kupitia Supa Jackpot bonus zake.

Wiki hii imeshuhudia washindi wawili wakijishindia zaidi ya milioni 15 ya bonus za Supa Jackpot.

Mshindi wa kwanza ni Oliveira Tarimo, huyu ni mkazi wa Iringa mjini, eneo linaloitwa Ihesa, yeye alijishindia kitita cha Sh. milioni 10.5 baada ya kubashiri kwa usahihi mechi 12 kati ya 13 za Supa Jackpot.

Mwingine ni Charles Kabwebwe, mkulima wa Alizeti kutoka Tabora yeye alijishindia kitita cha Sh. milioni 5.4 baada ya kubashiri kwa usahihi mechi 14 kati ya mechi 17 za Supa Jackpot za wiki iliyopita.

Wakizungumza katika ofisi za SportPesa, Oysterbay jijini Dar es Salaam, Oliviera alisema alianza kucheza na SportPesa miezi saba iliyopita, baada ya kuona marafiki, jamaa na ndugu zake wawili Aggrey na David wakicheza na kushinda kiasi cha Sh. milioni mbili.

"Mimi nilijifunza na kuanza kucheza na SportPesa Novemba 11, mwaka 2022. Nilikuwa nakaa na washikaji nawaona wanacheza muda mwingine walikuwa wanaongea namna walivyokuwa wanashinda au muda mwingine wamekosa labda mechi moja au mbili.

Sasa kilichonifanya nikaanza kucheza nakumbuka ilikuwa wakati wa kombe la dunia ambapo nina ndugu zangu mmoja anaitwa Aggrey na mwingine David. Hawa katika kipindi hicho walishinda milioni mbili," alisema Oliviera.

Naye Kabwebwe alisema kwa upande wake alianza kucheza na SportPesa miaka sita iliyopita.

"Mimi nilianza kucheza mwaka 2017, Nakumbuka wakati ule mimi nilikuwa bado nipo shule, sasa rafiki zangu karibu nane wote walikuwa wanapenda kubeti. Mara nyingi walikuwa wakipata hivi vihela vidogo vidogo vya kawaida.

Sasa si unajua wenzako wakishinda wanakuja kututambia na kutupa mizuka pengine na sisi au mimi naweza kucheza na kushinda hela kama wao. Ki ufupi kilichonivutia pia ni namna mtiririko wa washindi walivyokuwa wanatajwa, hasa hasa kwenye kurasa za mitandao ya kijamii na kwenye magazeti," alisema Kabwebwe.

Kuhusu mikeka yao ambayo imeshinda Oliviera anasema yeye aliweka mkeka wake siku ya Jumatano ya Tarehe 19 2023. Baada ya kuweka siku ya ijumaa alipata timu 8 kati ya timu 13. Siku iliyofuata yaani Jumamosi usiku wa Tarehe 22 alipata timu nne. "Kwanza mimi huwa na tabia ya kuweka zaidi ya mkeka mmoja katika kila Jackpot ya SportPesa. Nina wastani wa kuweka kuanzia mikeka mitatu mpaka mitano kila wiki.

Sasa unajua baada ya kuweka mikeka ile nilianza kuzifuatilia timu siku ya ijumaa. Kitu kizuri ni kwamba siku hiyo nilibahatika kupata matokeo kwenye timu nane. Ilipofika kesho yake sikufuatilia timu hata moja kwa kuwa nilikuwa bize sana.

Nakumbuka ilikuwa usiku nilipata sms ya hongera. Lakini muda ule sms inaingia sikuitilia maanani, kwakuwa nilikuwa nachati na watu kama watatu tofauti. Ilipopita muda wa kama dakika 40 hivi na ushehe nikakumbuka kuna sms iliingia ila sikuitilia maanani.

Aanaendelea kuelezea kuwa muda huo alikuwa amekaa na mwanae sebuleni na baada ya kuiona sms ile na kuthibitisha kwa macho kwamba ni milioni kumi na ushehe alinyanyuka kwa furaha kutoka kwenye kochi alilokuwa amekalia na kuanza kushangilia.

Naye Charles Kabwebwe anaelezea kuhusu mkeka wake wa Supa Jackpot ulioshinda, kwamba siku ambayo alibashiri aliweka jumla ya mikeka mitatu, lakini yeye hakusumbuka kuzifuatilia timu alizoziweka katika mikeka yake.

"Unajua mimi baada ya kuweka ile mikeka mitatu niliendelea na mishe zangu. Sikutaka kujipa presha, kufuatilia hizo timu. Nashukuru Mungu siku ya nne usiku baada ya kuwa nimeweka mikeka yangu nilipata sms ikinipa hongera kwa kushinda Supa Jackpot bonus kwa mechi 14 kati ya mechi 17.

Unajua sisi wa mikoa ya mbali na Dar-es-Salaam mzunguko wa hela sio mkubwa ki hivyo. Na hata matumizi yetu kwa siku, wiki na mwezi ni madogo. Kwa hivyo ilivyoingia sms ile ya Sh 5,423,697 ilinishtua sana.

Ilibidi niwasiliane na wazazi wangu na tushauriane. Nashukuru Mungu waliniunga mkono na leo nipo hapa kwenye uhakiki na makabidhiano wa mfano wa hundi na kutoa ushuhuda wangu.

Wote Oliveira na Charles wanawashauri watanzania kucheza na SportPesa hasa hasa jackpot zao kwani sio lazima mkeka wako ushinde kwa asilimia 100 ndio upate pesa.

Oliviera "Mimi napenda kuwaasa watanzania haijalishi umeshacheza kwa muda gani au umepoteza kiasi gani. Cha umuhimu ni kwamba tumia kiasi kidogo cha buku buku kila wiki kucheza hizi Jackpot na mambo yanaweza kukuendea vizuri kama mimi.

Charles "Mimi kwa upande wangu niwaambie wasikate tamaa. Kama ambavyo nilikuwa naona washindi wengine wakitangazwa na mimi leo nimetangazwa na kuingia katika historia ya washindi wa Jackpot bonus ya Supa Jackpot na wao wanaweza kushinda kama mimi. Hivyo wasichoke kubashiri.

Akiwapongeza washindi hao, Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano wa SportPesa, Sabrina Msuya, aliwataka wasibweteke na waendelee kucheza kwani wanaweza wakaja kushinda Jackpota kubwa au wakaendelea kushinda Jackpot bonus kwa viwango vya juu zaidi ya hivi walivyopata sasa.

"Niwaase tu kwamba ushindi huu usiwe ndio mwisho wa kucheza. Endeleeni kupambania mahela hayo yaliyopo kwenye Jackpot zetu. Si mnafahamu kwenye supa Jackpot kuna Jackpot mbali mbali za viwango tofauti," Msuya alisema.

Kuna ya mechi 17, 16,15,14 na 13. Jackpot zote hizi kila moja ina kiwango chake cha ushindi. Haufungwi na vigezo wala masharti kwani unaweza ukacheza zote kwa mpigo na ukapata ushindi au bonus kwenye Jackpot zote.Supa Jackpot wiki hii imesimamia 1,109,975,029.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAPILI - 07/05/2023

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 1878 | Aalborg vs Horsens | 1.69 | 3.65 | 4.76 |
| 13:15 | 4176 | Emmen vs Twente | 4.08 | 3.73 | 1.73 |
| 13:15 | 4363 | Almere City vs NAC Breda | 1.74 | 3.75 | 3.96 |
| 13:30 | 3731 | Atalanta vs Juventus | 2.30 | 3.21 | 2.91 |
| 14:00 | 1546 | Exeter vs Morecambe | 2.32 | 3.48 | 2.77 |
| 14:00 | 2206 | Sheffield Wed vs Derby | 2.48 | 3.39 | 2.63 |
| 14:00 | 2350 | Lincoln vs Shrewsbury | 1.97 | 3.58 | 3.43 |
| 14:00 | 2805 | Cambridge Utd vs Forest Green | 1.47 | 4.26 | 6.08 |
| 14:00 | 3743 | Barnsley vs Peterborough | 2.63 | 3.60 | 2.37 |
| 14:00 | 3902 | Fleetwood Town vs Ipswich | 6.48 | 4.66 | 1.41 |
| 14:00 | 4182 | Bristol Rovers vs Bolton | 2.83 | 3.44 | 2.29 |
| 14:00 | 4296 | Burton vs MK Dons | 3.44 | 3.44 | 2.00 |
| 14:00 | 4900 | Angers vs Monaco | 5.80 | 4.60 | 1.43 |
| 14:00 | 5348 | Portsmouth vs Wycombe | 2.06 | 3.49 | 3.24 |
| 14:00 | 5381 | Port Vale vs Plymouth | 3.99 | 3.79 | 1.77 |
| 14:00 | 5818 | Cheltenham vs Charlton | 2.49 | 3.47 | 2.57 |
| 14:30 | 1662 | Nurnberg vs Kaiserslautern | 2.12 | 3.29 | 3.29 |
| 14:30 | 5448 | KVC Westerlo vs Cercle Brugge | 2.64 | 3.32 | 2.47 |
| 14:30 | 5616 | Heidenheim vs Magdeburg | 1.64 | 3.94 | 4.65 |
| 15:00 | 2606 | Silkeborg vs Odense | 2.14 | 3.66 | 3.00 |
| 15:00 | 3160 | Lyngby vs Midtjylland | 3.45 | 3.71 | 1.94 |
| 15:30 | 5100 | GO Ahead Eagles vs Groningen | 1.67 | 3.79 | 4.38 |
| 15:30 | 5464 | SBV Excelsior vs Feyenoord | 9.81 | 6.41 | 1.20 |
| 15:30 | 5621 | Azam vs Simba | 4.85 | 3.12 | 1.55 |
| 16:00 | 1697 | Nantes vs Strasbourg | 2.65 | 3.25 | 2.47 |
| 16:00 | 2292 | AJ Auxerre vs Clermont Foot | 2.26 | 3.24 | 2.94 |
| 16:00 | 2848 | Torino vs Monza | 1.95 | 3.21 | 3.76 |
| 16:00 | 4202 | Malmo vs VAIK Football | 1.50 | 3.94 | 5.33 |
| 16:00 | 5190 | AC Ajaccio vs Toulouse | 3.15 | 3.30 | 2.13 |
| 16:00 | 5431 | Lorient vs Brest | 2.30 | 3.30 | 2.85 |
| 16:15 | 2035 | Hearts vs Celtic | 6.94 | 5.05 | 1.35 |
| 16:30 | 3693 | CSKA Moscow vs Gazovik Orenburg | 1.58 | 4.12 | 4.70 |
| 17:00 | 2501 | Rangers vs Aberdeen | 1.30 | 5.14 | 8.19 |
| 17:15 | 2132 | Parma vs Brescia | 1.71 | 3.35 | 4.81 |
| 17:15 | 4868 | Ponferradina vs Malaga | 2.89 | 2.94 | 2.47 |
| 17:30 | 1488 | FC Basel vs FC Zurich | 2.09 | 3.52 | 3.10 |
| 17:30 | 2118 | Maritimo vs Rio Ave | 2.28 | 3.12 | 3.07 |
| 18:00 | 1480 | RB Salzburg vs Rapid Vienna | 1.47 | 4.11 | 5.35 |
| 18:00 | 3828 | Zenit St Petersburg vs Spartak Moscow | 1.52 | 4.20 | 5.14 |
| 18:05 | 5032 | Lyon vs Montpellier | 1.62 | 3.96 | 4.51 |
| 18:30 | 1239 | Borussia Dortmund vs VfL Wolfsburg | 1.47 | 4.62 | 5.22 |
| 18:30 | 1859 | Newcastle vs Arsenal | 2.30 | 3.50 | 2.70 |
| 19:00 | 3185 | Giresunspor vs Fenerbahce | 5.24 | 4.40 | 1.50 |
| 19:00 | 4625 | Napoli vs Fiorentina | 1.87 | 3.47 | 3.75 |
| 19:30 | 2130 | Royal Antwerp vs Racing Genk | 2.25 | 3.32 | 2.95 |
| 19:30 | 4457 | Real Oviedo vs Zaragoza | 2.35 | 2.85 | 3.20 |
| 21:00 | 4710 | West Ham vs Manchester Utd | 3.11 | 3.39 | 2.11 |
| 21:45 | 3795 | Lecce vs Verona | 2.17 | 3.00 | 3.39 |
| 21:45 | 4331 | Troyes vs Paris St Germain | 6.66 | 4.99 | 1.35 |
| 22:30 | 2879 | Pacos Ferreira vs Sporting Lisbon | 7.04 | 4.73 | 1.37 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumapili Mei 7, 2023

Nipashe




## Lampard atoboa siri Chelsea

UKURASA 21




Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson (katikati mwenye miwani), akiwaongoza baadhi ya washiriki wa mbio, Mbeya Tulia Marathon msimu huu ambazo zimedhaminiwa na taasisi mbalimbali ikiwamo benki ya CRDB na Kampuni ya michezo ya kubashiri matokeo ya Betika zilizofanyika juzi na jana jijini, Mbeya. **PICHA: MTANDAO.**

# SIMBA SC, AZAM MECHI YA KISASI

**Na Faustine Feliciane**

### Makocha wafunguka wanalitaka Kombe la FA ili kupoza machungu...

HATUMWI mtoto dukani, unaweza kusema hivyo kuelekea mechi ya hatua ya nusu fainali ya mashindano ya Kombe la FA kati ya Azam FC dhidi ya Simba itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Nangwanda Sijaona ulioko mkoani, Mtwara.

**Mechi hiyo inaelezwa ni ya kulipiza kisasi baada ya Simba kulazimishwa sare na matajiri hao wa Chamazi katika mechi zote mbili za Ligi Kuu Bara msimu huu, huku Azam FC ikiwa na hasira ya kutolewa na Mnyama katika michuano ya msimu uliopita.**

Ugumu wa mchezo wa leo unatokana na ubora wa vikosi vyote viwili huku kila upande ukitaka kupambana kuhakikisha inajihakikishia kutwaa taji la michuano hiyo baada ya kushindwa kunyakua ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu.

Kocha wa Simba, Robert Oliveira 'Robertinho' ameweka wazi mikakati yake kuelekea katika mchezo huo kwa kujipanga kuizuia safu ya ushambuliaji ya Azam ambayo ipo chini ya straika Mzimbabwe, Prince Dube.

Robertinho alisema Dube amekuwa mwiba mkali katika michezo yote waliyokutana nao na kwa sababu hiyo amewapa kazi maalum mabeki wake kuhakikisha mshambuliaji huyo anadhibitiwa vizuri.

"Tuna matumaini makubwa katika mchezo huu, lakini tutachukua tahadhari zote kwa sababu utakuwa mchezo mgumu na tunacheza na timu bora pia, tumekutana nao kwenye ligi, tumeona ubora wao," alisema Robertinho.

Kocha huyo alisema amekiandaa vizuri kikosi chake na kila mchezaji atakayepata nafasi kucheza ameahidi kujitoa kwa ajili kusaka ushindi kutokana na umuhimu kuhitaji kusonga mbele katika michuano hiyo.

"Nitakuwa na mazungumzo zaidi na wachezaji wangu wote, naamini kwa kila mchezaji atakayepata nafasi ya kucheza atafanya kile kinachotakiwa ili kuipa timu ushindi na kusonga mbele, tunataka kufika hatua ya fainali," Robertinho alisema.

Naye Kocha wa Azam FC, Kally Ongalla, alisema wamemaliza maandalizi kuelekea mechi hiyo na kazi imebaki kwa wachezaji kwenda uwanjani kufanya kile walichoelekezwa.

Kally alisema wataingia kwa kazi moja ya kusaka ushindi kwa sababu wanahitaji kubeba kombe hilo msimu huu.

"Tunatamani kuwa sehemu nzuri ya kumbukumbu msimu huu, tunaenda kufika fainali kwa kuwaondoa Simba, naamini tutafikia malengo ambayo tumejiwekea, nafahamu ugumu wa mchezo huu lakini hiyo haitufanyi tuingie kinyonge kesho (leo)," alisema kocha huyo.

Azam ilifika hatua hiyo baada ya kuifunga Mtibwa Sugar mabao 2-0 huku Simba ikitoa kichapo cha bila huruma cha magoli 5-1 kwa Ihefu SC ya Mbarali, Mbeya.

Nusu fainali nyingine ya mashindano hayo itawakutanisha Singida Big Stars dhidi ya mabingwa watetezi, Yanga ambayo kwa sasa inajiandaa na mchezo wake wa hatua ya nusu fainali ya michuano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika kwa kuwakaribisha Marumo Gallants ya Afrika Kusini.

## Yanga watacheza fainali Afrika hivi...

**Na Saada Akida**

WASHAMBULIAJI wa Yanga, Fiston Mayele na Kennedy Musonda wametakiwa kujituma zaidi wanapokaribia lango la wapinzani kwa ajili ya kufunga mabao katika mechi ya hatua ya nusu fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Marumo Gallants itakayochezwa Mei 10, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, alisema lengo la kuwapa majukumu hayo mastraika wake ni kuhakikisha wanazitumia kwa faida dakika 90 za kwanza za hatua hiyo ya nusu fainali.

Nabi alisema anataka kuona timu yake inaimaliza mapema mechi yao kwa kufunga mabao ya kutosha ambayo yatawavusha kwenye hatua hiyo na kuweka rekodi kwa klabu na nchi.

Kocha huyo alisema hawataki kupata ushindi finyu ambao utawaweka kwenye presha na hivyo anawakumbusha washambuliaji wake kutumia vizuri kila nafasi watakayopata katika mechi hiyo ya kwanza.

Aliongeza siku zote hujifunza kutokana na makosa yao au watu wengine ambao husaidia kuwafanya waweke mikakati bora na hatimaye kufikia malengo waliyokuwa nao.

"Tumeliangalia kwa namna kubwa kwenye mchezo wetu wa hapa nyumbani, kuna mipango ya kupata matokeo ya mapema na idadi kubwa ya mabao ya kufunga yatasaidia kutuweka salama zaidi ikiwa wachezaji wajua wajibu wao.

Hatuhitaji kuona tunacheza kwa presha yoyote katika mchezo wetu wa hapa zaidi ya kuona safu ya ushambuliaji inatumia nafasi zote muhimu za kufunga katika dakika 45 kupindi cha kwanza na kipindi cha pili tusicheze kwa presha kubwa," alisema Nabi.

Aliongeza endapo watapata idadi nzuri ya mabao watakuwa katika nafasi salama ya kutocheza kwa presha kwenye mchezo wa marudiano huko ugenini kwa sababu watakuwa wanarudia makosa ya watani (Simba), zao ambao wameondolewa katika michuano hiyo ya CAF.

Kocha Mkuu wa Marumo Gallants, Dylan Kerr, aliliambia gazeti hili kikosi chake kitawasili nchini usiku wa kuamkia jumanne na wako tayari kwa ajili ya mchezo huo huku akitamba anaifahamu vizuri Yanga.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >